SUPA JACKPOT
TZS.1,065,505,647
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



BIMA YA AFYA KWA WOTE

**Serikali** yaonya haitotoa msamaha wasio na bima

UKURASA 5




Nipashe
Jumapili Januari 15, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581191
www.ippmedia.com
JUMAPILI
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 9



# Panga lafyeka vigogo wa CCM

UKURASA 2

## WANAOENDELEA/ WAPYA



Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo



Katibu mpya wa NEC, Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema

## WALIOTEMWA



Christina Mndeme



Dk. Abdulla Juma Saadalla 'Mabodi'



Ngemela Lubinga



Shaka Hamdu Shaka

## Watu 1,069 wauawa na wanyamapori

UKURASA 4



Mabaki ya gari aina ya Toyota Spacio baada ya kugongana uso kwa uso na lori (picha ndogo), eneo la Kwambe Point A Dumila, wilayani Kilosa mkoani Morogoro jana na kusababisha vifo vya watu wanne wa familia moja na wengine kujeruhiwa. **PICHA: IDDA MUSHI**



# Ajali ya gari ilivyoua wanne wa familia moja

UKURASA 4

MICHEZO **SIMBA: MASHABIKI JIANDAENI KUFURAHI** UK.24 **KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiongoza kikao cha kwanza cha Kamati Kuu mpya ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Panga lafyeka vigogo wa CCM

**Na Beatrice Shayo**

PANGA limefyeka vigogo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM). Kauli hiyo inasadifu mabadiliko makubwa ambayo Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya chama hicho imeyafanya katika sekretarieti.

Mabadiliko hayo yalitangazwa jana baada ya kumalizika kwa kikao cha NEC kilichofanyika jijini Dar es Salaam chini ya Mwenyekiti wa Taifa, Rais Dk. Samia Samia Suluhu Hassan. Katika mabadiliko hayo, wajumbe wawili tu wa Sekratarieti ya NEC ndio waliorejea katika nafasi zao huku wengine wakiondolewa.

Akitangaza mabadiliko hayo, aliyekuwa Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alisema Katibu Mkuu, Daniel Chongolo na Katibu wa NEC, Uchumi na Fedha, Dk. Frank Hawassi, wanaendelea kubaki katika nafasi hizo.

Wakati Chingolo na Dk. Hawassi wakibaki, Naibu Makatibu Wakuu, Christine Mndeme (Bara) na Abdallah Juma Sadalla 'Mabodi' (Zanzibar), wameondolewa kwenye nyadhifa hizo.

Wakuu wa idara, mbali na Shaka, wengine walioondolewa ni Dk. Moudline Castico (Oganaizesheni), Kanali Hezron Lubinga (Siasa na Uhusiano wa Kimataifa).

Hata hivyo, Mndeme, Shaka na Mabodi wanaendelea kuwa wajumbe wa NEC kutokana na ushindi walioupata katika uchaguzi uliofanyika wakati wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa CCM uliofanyika mwez i uliopita jijini Dodoma. Castico na Lubinga walibwagwa katika kinyang'anyiro cha ujumbe wa NEC.

Walioteuliwa kujaza nafasi za waliotemwa katika sekretarieti ni Anamringi Macha ambaye anakuwa Naibu Katibu Mkuu (Bara) na Mohamed Said Mohamed, maarufu kama Dimwa anayechukua nafasi ya Naibu Katibu Mkuu Zanzibar.

Makatibu na wakuu wa idara wapya walioteuliwa na nyadhifa zao kwenye mabano ni Sophia Mjema (Itikadi na Uenezi), Mbarouk Nassor Mbarouk (Siasa na Uhusiano wa Kimataifa) na Issa Haji Ussi, maarufu kama Gavu (Oganaizesheni).

Kabla ya uteuzi huo, Mjema alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga wakati Anamringi Macha ni ofisa mkongwe ndani ya CCM na aliwahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama. Katika uchaguzi wa kinyang'anyiro cha NEC, Macha aliibuka kidedea katika kundi la Tanzania Bara.

**KAMATI KUU MPYA**

Mbali na kufanya mabadiliko katika sekretarieti, NEC pia imeteua wajumbe sita kuunda Kamati Kuu (CC-NEC), watatu kutoka Zanzibar na wengine kutoka Tanzania Bara.

Walioteuliwa kwa Zanzibar ni Mohamed Aboud Mohamed, Mhandisi Nassir Ali Juma na Laila Burhan Ngozi. Aboud alishawahi kuwa Naibu Waziri wa Mambo na Ndani ya Nchi na baadaye iliyokuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika serikali ya awamu ya nne ya Tanzania kabla ya kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar.

Kwa upande wa Tanzania Bara, walioteuliwa ni Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda ambaye alikuwamo katika Kamati Kuu iliyomaliza muda wake, Hassan Wakasuvi na Halima Mamuya.

Mamuya aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) ambao ni moja ya Jumuiya za CCM pamoja na Mbunge wa Viti Maalum wa chama hicho.

**YAJAYO MAKUBWA**

Baada ya mabadiliko hayo ndani ya Chama, macho na masikio ya Watanzania ni kwa Rais Dk. Samia katika kuendelea kutekeleza ahadi yake ya kuisuka serikali kwa kufanya uteuzi kwenye nafasi mbalimbali.

Rais Samia aliomba rai kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa wa CCM kuwa anaomba kuisuka serikali ili kuteua watu watakaoendana na kasi yake ya kutaka kuwaletea Watanzania maendeleo.

Alianza kufanya hayo hivi karibuni baada ya kufanya mabadiliko makubwa ndani ya Ikulu baada ya kumteua Dk. Moses Kusilika kuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Kabla ya uteuzi huo, Dk. Kusiluka alikuwa Katibu Mkuu, Ikulu.

Dk. Kusiluka alichukua nafasi ya Balozi Hussein Katanga aliyeteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania, New York nchini Marekani na Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Ofisi za Umoja wa Mataifa, New York.

Rais Samia alimteua aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Kamishna Diwani Athumani kuwa Katibu Mkuu, Ikulu huku nafasi yake ikichukuliwa na Said Hussein Masoro ambaye kabla alikuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu na Mkurugenzi wa Shughuli za ndani wa idara hiyo.

Hata hivyo, uteuzi wa Diwani ulitenguliwa saa 43 baada ya kuteuliwa kwake na nafasi yake ikachukuliwa na Mulili Mahendeka, aliyekuwa ofisa mwandamizi Ikulu.

# Walimu 11,000 wabainika kuwa na utovu wa nidhamu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TUME ya Utumishi wa Walimu imesema jumla ya walimu 11,022 walipatikana na makosa mbalimbali ya kinidhamu, ikiwamo uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi, ukaidi na ulevi wakati wa saa za kazi katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2021/22.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa kikao cha kupitia ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Prof. Willy Komba, alisema makosa mengi yaliyobainika na wahusika kuchukuliwa hatua ni pamoja na utoro, kughushi vyeti vya kitaaluma, ukiukaji wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu.

Alifafanua kuwa kosa la utendaji kazi katika utumishi wa walimu lilihusisha walimu 1,290, akisisitiza kuwa hiyo si idadi ndogo kulinganisha na makosa mengine yaliyofanyika katika kipindi hicho.

Mwenyekiti huyo alisema katika kosa la uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi, ilibainika walimu wamekuwa wakikiuka taratibu za kimaadili kwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi wao kutokana na ukaribu.

"Kuwa na ukaribu na mwanafunzi siyo vibaya kwa kuwa unamwelimisha na kumpa elimu na maarifa lakini ukaribu unapopitiliza kwa mwanafunzi, hasa mwenye jinsia ya kike, tunajua tayari mwalimu ameshaweka uhusiano wa kimapenzi na tunapochunguza na kubaini hilo tunakuchukulia hatua kali ikiwamo ya kukufukuza kazi," alisema.

Mwenyekiti alifafanua kuhusu adhabu zinazotolewa kwa walimu wanapobainika kwenda kinyume cha maadili, inaanzia kwenye mamlaka ya nidhamu ngazi ya shule zinatoa adhabu kwa makosa mepesi, lakini zipo mamlaka za wilaya zinazotoa adhabu na mwalimu asiporidhika anakata rufani kwenda Tume ya Walimu.

"Idadi ya walimu 11,022 mashauri yao ndiyo yalisikilizwa na tume na ilitoa adhabu kulingana na uzito wa kosa walilotenda na sasa tunawataka wazingatie, wazifuate kanuni na wawe mfano bora kwa wanafunzi," alisema Prof. Komba.

Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume hiyo, Fatuma Muya, alisema lengo la kupitia ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu ni kuwaweka walimu waelewe ni mambo gani ya kufanya na yasiotakiwa kufanywa.

"Tunaona mwalimu ni mlezi wa wanafunzi na anatakiwa kuwa mwema kwa mwanafunzi na anatakiwa kumlea vizuri katika nyanja zote nne - anamlea kimwili, kisaikolojia, kiroho na kijamii na kuna mambo ya kimaadili hatakiwi kuyafanya, kwa mfano kujihusisha na wanafunzi kimapenzi, mwalimu huyo atachukuliwa hatua za kinidhamu," alisema Muya.

Alisema tume ni mamlaka ya ajira kwa walimu na pia ni mamlaka ya kinidhamu na endapo mwalimu atakiuka maadili, atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwamo kupoteza ajira.

Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu alisema baada ya kukamilika kwa kazi hiyo ya kuandaa kanuni, tume hiyo itachapisha vitabu na kuvisambaza, pia itatoa elimu kwa ngazi mbalimbali kwa walimu ambao watanufaika na kufanya shule kuwa mahali salama.

Akifunga kikao kazi hicho cha siku nne, Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia Elimu Mkoa wa Morogoro, Germana Mung'aho, alisema ufafanuzi wa kanuni hizo umefanyika kwa kuzingatia mabadiliko ya kisera, sheria, kanuni, utandawazi na ongezeko la walimu.

Aliitaka tume hiyo kuwajengea uwezo walimu na kuweka utaratibu wa ufuatiliaji wa kuona namna walimu wanavyozingatia kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu.

"Nina imani tutakapotekeleza haya tutakuwa na walimu wenye kuzingatia kanuni za maadili ya kazi yao na hivyo tutaweza kupiga hatua ya kuwa na shule za msingi zinazozingatia mpango wa shule salama," alisema Mung'aho.

HABARI KITAIFA

# Vigogo Zanzibar watua Mahakama ya Mafisadi

**Na Kulwa Mzee**

VIONGOZI waandamizi wa Mahakama Kuu Zanzibar wametembelea Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa lengo la kujifunza jinsi mahakama hiyo inavyofanya kazi.

Viongozi hao ambao ni Mtendaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Kai Mbaruk na Mrajisi wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Valentina Katema, walitembelea mahakama hiyo jana na kukutana na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Elinaza Luvanda, Naibu Msajili, Magdalena Ntandu na Mtendaji wa Mahakama hiyo, Masalu Kisasila.

Naibu Msajili, Ntandu aliwaeleza viongozi hao kuwa mahakama hiyo ni moja kati ya divisheni nne maalum za Mahakama Kuu ya Tanzania zilizoanzishwa kwa sababu mahsusi za utoaji haki na mazingira bora ya kuvutia uwekezaji katika kukuza na kujenga uchumi nchini.

"Lengo ni kuharakisha utoaji wa haki ili kuvutia na kuweka mazingira bora na wezeshi ya uwekezaji kiuchumi nchini, kuongeza imani kwa wawekezaji, kujenga na kuinua uchumi imara wenye kuhimili ushindani na hatimaye kuleta maendeleo ya jamii nchini," alisema.

Alibainisha kuwa mahakama hiyo, maarufu Mahakama ya Mafisadi, imepewa mamlaka ya kusikiliza mashauri ya makosa ya rushwa na uhujumu uchumi ambayo thamani yake au kiwango cha fedha ni kuanzia Sh. bilioni moja na kuendelea na ina mamlaka pia ya kusikiliza makosa yote yaliyoorodheshwa katika Jedwali la Sheria ya Uhujumu Uchumi yanayoangukia katika vifungu vya sheria mbalimbali zilizoko kwenye jedwali hilo bila kujali thamani au kiwango cha fedha.

"Mahakama hii ina Masijala Kuu moja iliyoko Dar es Salaam na Masijala zingine ndogo zilizoko kila penye Kanda ya Mahakama Kuu ambazo ni Dodoma, Morogoro, Tanga, Mwanza, Shinyanga, Sumbawanga, Kigoma, Bukoba, Mbeya, Arusha, Moshi, Mtwara, Songea, Iringa, Musoma na Tabora.

"Mahakama inapokea na kuendesha mashauri nchi nzima kuanzia Masijala Kuu isipokuwa kwa mashauri ya maombi ya dhamana ambayo husikilizwa na kuamuliwa kwenye kanda husika.

"Mashauri yanayosajiliwa katika divisheni hii ya Mahakama Kuu yanaendeshwa kwa mujibu wa kanuni zilizotolewa na Gazeti la Serikali Namba 267 la Mwaka 2016.

"Kwa mujibu wa kanuni hizi, ukomo wa muda wa kusikiliza mashauri katika divisheni hii ni kipindi kisichozidi miezi tisa tu tangu kuwasilishwa kwa taarifa ya mashtaka," alisema Ntandu.

Alisema hadi sasa divisheni imefanikiwa kumaliza mashauri 706 ya uhujumu uchumi na maombi ya dhamana, hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika utatuzi wa migogoro kwenye jamii na kuleta utulivu na amani.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas (kushoto), akizungumza baada ya kuzindua upandaji miti katika Shule ya Sekondari Ruhuwiko, wilayani Mbinga mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki ya Dunia yakoshwa utekelezaji mradi BOOST

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

BENKI ya Dunia ambayo ni mfadhili wa Mradi wa BOOST, imeonesha kuridhishwa na namna Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inavyotekeleza moja ya malengo ya mradi huo katika kuwasaidia walimu kuwa na mwenendo mwema unaozingatia miiko na maadili ya kazi hiyo.

Hayo yalibainishwa na Mtaalamu wa Elimu kutoka Benki ya Dunia ambaye ni Msaidizi Mkuu wa Mradi wa BOOST, Gemma Todd wakati wa Kikao Kazi kilichoandaliwa na TSC kwa lengo la kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika Januari 10-13 mjini hapo.

Alisema Mradi wa BOOST unalenga kuimarisha na kuboresha elimu ya awali na msingi kwa shule za serikali ambapo shughuli mbalimbali zimepangwa kufanyika ili kufikia lengo hilo.

Shughuli hizo ni kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, kuhakikisha shule zina usalama wa kutosha, kujenga shule mpya na madarasa mapya na kuhakikisha walimu wanapata mafunzo mara kwa mara na kwa karibu.

"Nimeshiriki kwenye warsha nzuri sana ambayo imeandaliwa na TSC kujadili maadili ya walimu wetu, tunajua watoto watashindwa kusoma wasipokuwa na usalama shuleni, pia wasipokuwa na walimu ambao wanaweza kuwa karibu nao na kuweza kuwaongoza vizuri.

"Kwa kweli warsha hii imekwenda vizuri na matokeo ya warsha hii ni kutusaidia kufikia malengo ya afua namba mbili ya mradi wetu ambayo inazungumzia shule salama," alisema Todd.

Alisema kuwa katika mazingira ya sasa ambapo kumekuwa na mabadiliko ya kitabia yanayosababisha kuharibika kwa maadili katika jamii, ni muhimu kuweka mkazo katika kusaidia walimu kuzingatia miiko na maadili ya kazi yao ili kufanya shuleni kuwa mahali salama kwa wanafunzi, hivyo TSC imefanya jambo la msingi kwa kuamua kufanya mapitio ya ufafanuzi wa maadili na utendaji kazi wa walimu.

"Kanuni za Maadili hayo zikifafanuliwa vizuri na kueleweka zitamwongoza mwalimu kutambua wajibu wake awapo shuleni au eneo lake la kazi kwa kuwa wajibu wake ni zaidi ya kufundisha darasani.

"Mwalimu anawajibika katika malezi ya mtoto kimwili, kiakili, kiroho, kijamii na kisaikolojia. Lakini pia ana wajibu kwa viongozi wake na wasimamizi wake wa kazi, anawajibika kwa jamii anamoishi na anawajibika kwa umma au taifa kwa ujumla. Haya yote yamejadiliwa kwa kina katika warsha hii," alisema.

# RC atangaza 'vita' dhidi wanaokata miti hifadhini

**Na Gideon Mwakanosya,** MBINGA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, amesema kuanzia sasa anatangaza vita endelevu na watu wote wanaokata miti kwenye misitu na wanaoharibu vyanzo vya maji.

Alitangaza vita hiyo juzi kwa nyakati tofauti wakati anazindua upandaji wa miti shuleni kwenye wilaya za Mbinga na Nyasa.

Kanali Thomas aliwaagiza wakuu wote wa wilaya, wakurugenzi, maofisa tarafa, kata na vijiji kusimamia sheria mama ya mazingira ili kulinda misitu na vyanzo vya maji. "Wilaya ya Mbinga inaongoza kwa kuharibu misitu na kuacha milima ikiwa vipara, ninyi kila mahali mnapoona miti mnatembea na shoka na kuteketeza miti, muone aibu mna ugomvi gani na miti" Kanali Thomas alihoji.

Alisisitiza kuwa anaanzisha ugomvi na wakata miti na wanaoharibu vyanzo vya maji kutokana na kufanya shughuli za kibinadamu hadi ndani ya vyanzo vya maji.

Aliongeza kuwa amebaini maeneo mengi yenye hifadhi za misitu zikiwamo hifadhi ambazo zipo chini ya Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na kwenye vyanzo vya maji na maeneo ya misitu ya vijiji, yanavamiwa na miti yake kukatwa, hivyo anawaagiza wadau wote wa mazingira kuyalinda maeneo hayo kikamilifu.

Aliagiza miti yote inayopandwa itunzwe ili ikue na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yaliyoanza kuleta athari katika baadhi ya maeneo ikiwamo mito na vyanzo vingine vya maji kukauka na kukosa mvua ya uhakika.

Kanali Thomas alisema upandaji miti na kulinda vyanzo vya maji iwe ni kampeni ya kudumu, akisisitiza kuwa ameamua kuzindua kampeni ya kupanda miti katika shule ili kujenga tabia ya kupenda kupanda miti kwa watoto kuanzia shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati hadi vyuo vikuu.

Mkuu wa Mkoa pia aliiagiza TFS kuhakikisha kila shule mkoani Ruvuma inapewa miche ya miti ya kutosha kwa ajili ya kupanda kwenye mazingira yao.

Awali akitoa taarifa ya upandaji miti katika Wilaya ya Mbinga kwa kipindi cha mwaka 2022/23, Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Aziza Mangosongo, alisema wilaya hiyo ina misitu mitano ya hifadhi ambayo ni Namswea, Liwiliktesa, Kigonsera, Amanimakoro na Lupembe.

Aziza alisema wilaya hiyo pia ina mashamba ya miti ya kupandwa ambayo ni Mbambi, Ugano, Likopesi, Ndengu, Mpapa, Lubela, Mahenge na Mbuji na kwamba misitu hiyo inasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya na serikali kuu.

"Uzinduzi wa upandaji miti katika shule ni kielelezo cha upandaji miti katika Wilaya ya Mbinga ambao unakwenda sanjari na ugawaji wa miche ya miti kibiashara iliyooteshwa na TFS," alifafanua.

Alibainisha kuwa TFS katika Wilaya ya Mbinga imezalisha miche ya aina mbalimbali 208,650. Kati yake, misindano 67,120, misaji 9,650, mibolea 13,020, mikaratusi 121,838, miembe 300, michungwa 200, parachichi 500, mikangazi 800 na misedelela 300. Katika wiki maalum ya upandaji miti mkoani Ruvuma iliyoanzia Januari Mosi hadi juzi, jumla ya miche ya miti ya asili 1,100,000 iliyotolewa na TFS imepandwa.

# Watu 1,069 wauawa na wanyamapori nchini

**Na Jenifer Gilla**

IMEBAINISHWA kuwa vifo vya watu 1,069 vimetokea huku wengine 642 wakijeruhiwa na kupata ulemavu wa kudumu katika kipindi cha miaka saba kutokana na migogoro kati ya wananchi na wanyamapori inayoendelea kwenye maeneo yanayounganisha hifadhi (shoroba) mbalimbali nchini.

Vilevile, takribani hekta 41,404 zilizokuwa zinatumika kwa kilimo zimeharibiwa huku mifugo 792 ikiliwa na wanyamapori kufuatia migogoro baina ya makundi hayo katika kipindi hicho kilichoanzia mwaka 2012-2019.

Hayo yalibainishwa juzi wilayani Bagamoyo mkoani Pwani na Meneja Ufuatiliaji na Tathmini wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari za mazingira yaliyotolewa na Chama cha Waandishi wa Mazingira (JET) kupitia Mradi wa Tuhifadhi Maliasili.

"Takwimu zilizotolewa na Idara ya Wanyamapori zinaonyesha kuwa wamelipa fidia ya takribani Sh. bilioni 4.6 kwa watu ambao wameathirika kwa namana moja au nyingine na migogoro hiyo, jambo ambalo linaitia hasara serikali," alisema John.

Meneja Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi wa Mradi wa huo, Dk. Elikana Kalumanga, alisema chanzo kikuu cha migogoro ni kuwapo kwa shughuli za kibinadamu kwenye njia zinazotumiwa na wanyamapori wakitoka sehemu moja kwenda nyingine (shoroba) ikiwamo kilimo na ufugaji.

Dk. Kalumanga alisema shoroba hizo zimekuwa zikiathiriwa na shughuli hizo za binadamu na kuhatarisha kuwapo maeneo hayo na maisha ya wanyama hao kwa ujumla.

"Kwa sasa hali za shoroba zetu mbalimbali nchini si nzuri kwani kwa mujibu wa takwimu za serikali zipo baadhi zimepotea kabisa kutokana na shughuli hizo za wananchi zinazofanywa kila siku, ndiyo maana tunatoa mafunzo haya kwa waandishi wa habari ili watusaidie kutoa elimu kwa jamii juu ya madhara na umuhimu wa kutunza shoroba hizi," alisema Dk. Kalimanga.

Akifungua mafunzo hayo, Mkurugenzi wa JET, John Chikomo, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo ili kuwapatia waandishi habari elimu na kuongeza idadi ya watakaotoa taarifa juu ya uhifadhi wa maliasili ya taifa. "Tulifanya uchunguzi na tukagundua kuwa kuna waandishi habari wa uhifadhi wachache nchini na sababu kubwa ni kuwa wengi wao hawana uelewa juu suala hilo, hivyo hawajui waanzie wapi. Kupitia mafunzo haya tunategemea kuanzia sasa kuona habari nyingi za uhifadhi maliasili," alisema John.

Mmoja wa waandishi waliohudhuria mafunzo hayo, Janeth Jovin alisema kupitia mradi huo amepata elimu juu ya uhifadhi maliasili ikiwamo vyanzo vya migogoro hiyo, namna ya kuandika habari hizo na wapi atapata takwimu, jambo lililompa hamasa ya kuandika habari za uhifadhi.



Mmoja wa majeruhi wa ajali hiyo, akiwa amelazwa katika Kituo cha Afya St. Joseph Dumila, jana. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Wanne wa familia moja wafa katika ajali ya gari

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WATU wanne wa familia moja wamefariki dunia na wengine wawili kujeruhiwa baada ya gari dogo walilokuwa wakisafiria kugongana uso kwa uso na lori kwenye eneo la Kwambe Point A Dumila wilayani Kilosa mkoani Morogoro.

Ajali hiyo iliyotokea jana ilisababisha foleni ya magari kuanzia majira ya saa tatu asubuhi.

Ajali hiyo ilihusisha lori lenye namba za usajili T 418 DDP lililokuwa linatoka Dar es Salaam kwenda Mwanza na gari ndogo aina ya Toyota Spacio lenye namba T 162 DGN ambalo.

Dereva wa lori lililohusika na ajali aliyekuwa eneo la tukio, Samir Halfan Ally alidai ajali hiyo imesababishwa na dereva wa gari dogo ambaye ni mwanamke aliyekuwa akiendesha kwa mwendo kasi na hivyo kushindwa kumkwepa.

Kwenye Kituo cha Afya St. Joseph Dumila, Mganga Mfawidhi wake, Dk. Manyele Kapongo alisema walipokea miili ya watu wanne ambao ni watu wazima wawili, binti na mtoto mdogo.

Alisema walipokea majeruhi wawili ambao ni mama na mtoto wake.

"Mmoja tumempeleka kwenye X-ray, analalamikia zaidi maumivu ya mgongo," alisema Dk. Kapongo.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Alhaj Majid Mwanga, aliyefika eneo la ajali na baadaye hospitalini, alisema tayari wametambua mwili wa mwanamke aliyekuwa akiendesha gari hilo na ambaye ndiye alikuwa kiongozi wa familia hiyo na kwamba ni mtumishi wa umma.

"Tunafanya taratibu zaidi kuwasilisha ndugu, wafike kumthibitisha na kuchukua miili ya waliofariki dunia kwa ajali na sisi tunaendelea kuhakikisha majeruhi walioko hospitalini wanapata huduma ipasavyo, tunatoa pole kwa wote walioguswa na ajali hii," alisema Mwanga.

Alitoa wito kwa madereva kuzingatia sheria na kanuni za usalama barabarani ili kuepuka ajali zisizo za lazima ambazo nyingi husababishwa na uzembe, hivyo kugharimu maisha ya watu na mali zao.

# Watumishi halmashauri kortini tuhuma za wizi

**Na Neema Hussein,** KATAVI

JESHI la Polisi Mkoa wa Katavi limewafikisha mahakamani watu 11, akiwamo Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, Shinda Ndege (33) kwa tuhuma za wizi wa maboksi 139 ya marumaru, mali ya Hospitali ya Wilaya ya Mlele.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame, alisema kukamatwa kwa watuhumiwa hao kumetokana na msako na doria za jeshi hilo kuzuia uhalifu ndani ya mkoa.

Aliwataja watuhumiwa wengine ni Tovatus Biseko (29), Hamis Msukuma (28), Godfrey Eneah (26), Paul Kizito (30), Daud Mlegea (24), Tambwe Shabani (31), Jafari Ramadhani (24), Vitalis Simon (29), Abdallah Kassim (22) na Musa Hamis (30).

Alisema mtumishi huyo ambaye ni Ofisa Mifugo anadaiwa kuchukua vigae hivyo na kwenda kujenga kwenye chumba chake cha biashara.

Katika tukio lingine, jeshi hilo linawashikilia watu wawili ambao ni Sweetbert Kanumba (26) na Mathias Amos (39) kwa tuhuma za kudaiwa kuiba mifuko 14 ya saruji ambayo ni mali ya Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) wilayani Mlele.

Mbali na tukio hilo, pia wanamshikilia mtu mmoja aliyetambulika kwa jina la Gisbert Simon (40), mkazi wa Kasimba kwa tuhuma za kudaiwa kuiba 'televisioni', king'amuzi na mzani wa kupimia uzito watoto, vyote mali ya Kituo cha Afya Kasekese, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika.

Kamanda Makame alisema hawatoshindwa kumchukulia hatua mtu yeyote anayejihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi wa miradi ya serikali kwa kuwa serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya kupeleka huduma kwa wananchi.

Watuhumiwa wote wanaendelea kuhojiwa na Jeshi la Polisi na mara baada ya upelelezi kukamilika, watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

# Serikali yaonya haitotoa msamaha wasiokuwa na bima

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imesema itasimama kidete kuhakikisha kila Mtanzania anafahamu umuhimu wa kuwekeza na kuweka kipaumbele kwenye afya, ikionya kuwa hakutakuwa na msamaha wowote baada ya Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote kupitishwa bungeni.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitoa angalizo hilo jana mkoani Dar es Salaam baada ya kutembelea Hospitali ya Dar Group iliyoko eneo la Tazara ambayo imepatiwa hadhi ya kutoa matibabu ya moyo hususan kwa watoto wenye umri wa miaka 15.

Alisema ajenda kuu iliyoko mbele ya sekta hiyo ni huduma Bora na bima ya afya kwa wote, ambayo kwa sasa kiwango kinachotazamiwa ni kati ya Sh. 340,000 hadi 360,000 kwa mwaka kuhudumia watu sita kwa huduma za rufani, kanda na za kibingwa.

Pia alisema kutakuwa na kundi lingine kwa ajili ya matibabu ya kuanzia ngazi ya kituo cha afya hadi hospitali za wilaya kwa malipo ya Sh. 66,000 kwa mwaka bila kuhusisha matibabu ya rufani na kibingwa.

"Watanzania lazima wajifunze kuwekeza katika afya. Bunge litakapopitisha muswada wa bima ya afya kwa wote, hakutakuwa na nisamehe.

"Ninajisikia aibu, mnaotoa huduma bora, lakini hapo hapo Watanzania wananifuata 'waziri maiti imezuiwa, imezuiwa! Nami siwezi kusema isitoke, ibaki.

"Niacheni nipitishe sheria, hatutaoneana huruma, wasiokuwa na uwezo tutawabainisha. Kiwango cha bima ya afya mtu ataamua alipie Sh. 66,000 kwa mwaka aishie ngazi ya wilaya, akapata dawa zote, vipimo au ulipie hiyo Sh. 360,000 ufike hospitali za rufani, kanda, ya Taifa Muhimbili, JKCI.

"Katika maisha ya binadamu yeyote, hakuna kitu muhimu kama afya, bila afya huwezi kufanya elimu, ulinzi. Tutasimama kidete, kuhakikisha kila Mtanzania anajua umuhimu wa kuwekeza katika afya," alisema Ummy.

Alisema serikali imeiteua rasmi Hospitali ya Dar Group kuwa kituo cha matibabu ya moyo chini ya Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) hususan kwa matibabu ya watoto chini ya miaka 15.

"Awali hospitali hii ililenga wafanyakazi wa viwandani lakini Novemba mwaka jana, serikali iliichukua hospitali hii ili kuiendesha. Nilitafakari kuwa niipe hadhi gani hospitali hii baada ya kuichukua, nikaona kuna ongezeko la mahitaji ya matibabu ya wagonjwa wa moyo hasa Dar es Salaam.

"Nikaamua sasa kuwapa JKCI ili kuiendesha na ndani ya miezi miwili, sijutii uamuzi wangu. Idadi ya wagonjwa imeongezeka. Hapa iwe kwa ajili ya matibabu ya watoto chini ya miaka 15," alisema Ummy.

Waziri huyo aliipongeza JKCI kwa kuwa kati ya taasisi ambayo inazingatia maadili na kuwa kati ya kituo cha huduma za afya kinachojisimamia vyema, ikiwamo kutojihusisha na vitendo vya rushwa.

"Malalamiko ninayoyasikia JKCI, ni gharama kubwa, sio kuhusu rushwa kwa takribani miaka sita nikiwa hapa, ninatamani hospitali zote ziige huduma kama za taasisi hii, inajiendesha vizuri," alipongeza.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Dk. Peter Kisenge alisema hatua hiyo imekuja baada ya kubaini ongezeko la wagonjwa wa aina hiyo makao makuu ya JKCI na kuamua kusogeza huduma Hospitali ya Dar Group hususan kwa wafanyakazi wa viwandani wa eneo hilo.

Dk. Kisenge alisema eneo hilo pia litajengwa jengo la kubwa kwa ajili ya kutoa huduma hiyo, hasa kuwahudumia watoto, ingawa na kwa rika lingine huduma zitapatikana.

"Kuanzia sasa hapa Dar Group huduma zitaanza za moyo na nyinginezo, tumeshawaleta madaktari bingwa wa moyo na vifaa vya zaidi ya Sh. milioni 500 na vimefungwa. Wananchi wote eneo la Temeke watapata huduma," alisema Dk. Kisenge.



Wananchi wakimdhibiti kijana (wa pili kulia), aliyetuhumiwa kuiba mfuniko wa jenereta, eneo la Buguruni, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# 'G20 toeni fedha kukabili mabadiliko ya tabianchi'

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, amewaomba wajumbe wa nchi zenye uchumi mkubwa duniani (G20) kutoa fedha ili kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na usalama wa chakula.

Naibu Waziri huyo alitoa kauli hiyo juzi katika mkutano wa siku mbili uliofanyika katika Mji Mkuu wa India, New Delhi, akishiriki kwa njia ya mtandao.

Taarifa iliyotolewa na Ubalozi wa India nchini jana, ilibainisha kuwa katika mpango mpya na wa kipekee, India imeandaa mkutano huo maalum wa mtandaoni ambao ulishirikisha mawaziri kutoka nchi mbalimbali ulimwenguni.

Walioshiriki katika mkutano huo ni mawaziri wa fedha, mazingira, mambo ya nje, nishati, afya, elimu, biashara na mawaziri wakuu na zaidi ya nchi 120 zilizoshiriki.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa mkutano huo pia ulihudhuriwa na Waziri Mkuu wa India, Shri Narendra Modi.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa India itahakikisha hoja zote na mapendekezo yote yaliyotolewa na nchi washirika katika mkutano huo, yanafanyiwa kazi kwa utambuzi wa kimataifa.

Ilisema kuwa urais wa G20 wa India unaoendelea unatoa fursa maalum kwa nchi ambazo siyo wanachama wa nchi zenye uchumi mkubwa duniani kubadilishana mawazo na matarajio yao kwa nchi za G20.

Taarifa ya Waziri Mkuu wa India inasema "Urais wa G20 wa India utaundwa kwa mashauriano ambayo siyo tu kwa washirika wa G20, lakini kwa wasafiri wa kusini mwa dunia ambayo sauti yao mara nyingi huwa haisikiki."

# Serikali yatoa angalizo matapeli Sekta ya Fedha

**Na Beatrice Moses**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewataka wananchi wa kada mbalimbali kuepuka kutapeliwa fedha kwa kuhakikisha wanawekeza kwenye taasisi za kifedha zinazoaminika.

Alitoa angalizo hilo jana jijini Dar es Salaam katika salama zake wakati wa uzinduzi rasmi wa Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja Faida Fund, hotuba yake ikisomwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma ma Utawala Bora, Jenista Mhagama.

Katika uzinduzi huo, Waziri Mhagama alisema matarajio ya wananchi ya kujiendeleza kiuchumi yatafanikiwa iwapo watawekeza fedha zao kwenye maeneo salama.

"Uwekezaji unaofanywa kwenye mfuko wa Faida Fund ni sehemu ya kutekeleza maagizo ya serikali ikiwamo kuwajengea uwezo wa kiuchumi wananchi," alisema.

Alihamasisha vikundi mbalimbali vikiwamo vya wanawake, watu wenye ulemavu na vyama vya siasa na michezo kuwekeza kwa pamoja kwa kadri ya viwango wanavyomudu.

Waziri Mhagama alisema Faida Fund ipo chini ya Watumishi House Investments (WHI) ambayo pia inamiliki Mfuko wa Nyumba ulioonyesha mafanikio.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa WHI, Hosea Kashimba, alisema mwitikio wa uwekezaji ni mzuri kwa kuwa awali walitarajia kuuza vipande vya Sh. bilioni 7.5 walipoanza kuuza Novemba Mosi mwaka jana lakini wamefanikiwa kuuza vya Sh. bilioni 13.5. Mauzo hayo yanatarajiwa kufika Sh. bilioni 20 ifikapo Juni mwaka huu.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Natu Mwamba alisema serikali ina mikakati ya dhati kuhakikisha mpango huo unaleta maendeleo kwa watu unatekelezwa kwa mafanikio.

Alisema mfuko huo unakidhi mahitaji ya uwekezaji wa makundi mbalimbali, hivyo ukitumiwa vyema na wananchi, utasaidia kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwan Kikwete, alitumia nafasi hiyo kuwataka wananchi kuzingatia mipango miji katika ujenzi wa nyumba.

"Maendeleo yanakwenda na mipango miji ikiwamo matumizi mazuri ya maeneo," alisema Ridhiwani.

Mkurugenzi wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, ambao ndiyo watunza dhamana ya mfuko huo, alisema ni salama kwa wawekezaji na unatumia mfumo wa kisasa wa ununuzi wa vipande, hatua ambazo zinawapa wepesi wawekezaji.

Nsekela aliahidi benki yao itahakikisha inatoa elimu kupitia matawi yake nchini, wananchi watambue umuhimu wa kuwekeza kwa pamoja na faida zilizoko, ikiwamo kuwaendeleza kiuchumi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari zichukuliwe mvua zinazoendelea ili zisisababishe maafa

**HIVI** sasa mvua kubwa zinaendelea kunyesha maeneo mbalimbali nchini ambazo kwa upande mmoja ni neema na upande mwingine ni maafa kwa baadhi ya maeneo.

Tunasema ni neema kutokana na imani kwamba mvua hizo zitatumika katika kilimo hivyo mazao kupatikana kwa wingi tofauti na mwaka jana nchi ilipokumbwa na ukame na kusababisha maeneo mengi hasa Dar es Salaam na Pwani kukosa maji ya uhakika na kuwapo kwa mgawo wa umeme. Sambamba na hayo, kulikuwa na uhaba wa mazao ya chakula hali iliyofanya mfumuko wa bei hasa kwa vyakula kuwa juu.

Aidha, mvua hizo ni kilio kwa baadhi ya maeneo kutokana na kuathiri baadhi ya kaya katika mikoa kwa sababu ya mafuriko. Katika mkoa wa Morogoro, mathalan, takribani kaya 48 zimeathirika na mafuriko kutokana na mvua kubwa iliyonyesha Alhamisi usiku.

Wananchi hao katika Manispaa ya Morogoro, wamelazimika kuyakimbia makazi yao baada ya kutokea mafuriko. Licha ya kuyakimbia makazi, pia wanahitaji misaada ya kibinadamu baada ya vyombo vyao na vyakula kuzolewa na maji yaliyoingia katika nyumba zao na kuharibu mali.

Kutokana na kuwapo kwa maafa hayo na mvua hizo zimeanza tu kunyesha, ni dhahiri kwamba kuna uwezekano mkubwa kuwa zitaendelea kunyesha na kusababisha adha kwa wananchi katika maeneo mbalimbali.

Kama ambavyo Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imekuwa ikitangaza kuwapo kwa mvua hizo, kuna maeneo mbalimbali ambayo yanaweza kukumbwa na mafuriko. Kwa mantiki hiyo, wananchi wanatakiwa kufuata maelekezo yanayotolewa na TMA ili kujilinda na maafa yanayoweza kutokea kutokana na mvua hizo.

Mafuriko yaliyotokea Morogoro na kusababisha maafa kwa baadhi ya wakazi, yanapaswa kuwa somo kwa Watanzania wote kuwa wanapaswa kuchukua tahadhari ili kutokukumbwa na adha hiyo, hivyo kupoteza mali pamoja na maisha kwa ujumla.

Kwa wale wanaoishi maeneo ya mabondeni kwa mfano, wanapaswa kuhakikisha mikondo ya maji na mifereji inazibuliwa ili kuruhusu maji ya mvua kupita kwa urahisi. Katika mkoa wa Dar es Salaam, kwa mfano, mifereji ya maji machafu pamoja na mito imejaa taka nyingi kiasi kwamba mvua zikinyesha maji hayapiti kwa urahisi na matokeo yake kuvamia kuvamia makazi ya watu na hatimaye kusababisha maafa.


Mvua kubwa kama hizi pia husababisha miundombinu ya usafirishaji kama barabara kuharibika na kuwafanya abiria wanaosafiri kwa mabasi kukwama hasa maeneo ambayo barabara zake si za lami. Hata zile za lami, katika baadhi ya maeneo madaraja huharibika, hivyo kukosekana kwa mawasiliano katika ya sehemu moja na nyingine.

Licha ya wananchi kuchukua tahadhari, ni vyema pia taasisi za serikali zilizopewa dhamana ya kusimamia masuala ya maafa hasa Idara ya Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kamati za maafa za wilaya na mikoa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, zikajiandaa kisaikolojia dhidi ya majanga yanayoweza kutokea kutokana na mvua hizi ili kuwasaidia waathirika katika sehemu mbalimbali za nchi.

Kama wahenga wasemavyo bora kuzuia kuliko kutibu, ni vyema taasisi hizi zikajiandaa kudhibiti pia athari za mafuriko badala ya kusubiri yatokee na kusababisha upotevu wa mali na maisha ya watu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Ukatili wa kijinsia una madhara mengi, tuutokomeze

**VITENDO** vya ukatili wa kijinsia, vinatajwa kuwa na madhara mengi ambayo manusura inaweza kudumu nayo kwa muda mrefu. Madhara hayo yakiwamo ya kiafya, kisaikolojia na kimwili, yanaweza kuharibu fursa ya mtu kuishi maisha yenye mafanikio.

Athari hizo zinaweza kusababisha mtu kushindwa kushiriki masuala ya kiuchumi na uwezo wa kuboresha maisha ya familia.

Kwa upande wa watoto, vitendo vya ukatili wa kijinsia vinaathiri ukuaji wa ubongo wao, wanapopatwa au kushuhudia vitendo hivyo na kwamba nafasi yao ya kukua kimwili na kiafya inaathirika na inawezekana wasifanye vizuri darasani.

Kutokana na athari hizo na nyingine, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa kupinga vitendo hivyo, imekuwa ikifanya kila njia kuhakikisha ukatili si sehemu ya maisha ya kila siku ndani ya jamii.

Imekuwa ikitoa elimu ya kuzuia ukatili katika jamii kwa lengo la ustawi bora wa wanawake na watoto ambayo kimsingi ni taifa la kesho na ndio maana hivi karibuni kulikuwa na timu iliozunguka mikoani kutoa elimu.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WilDAF) na Mtandao wa Kupinga na Kupambana na Ukatili imekuwa ikifanya kampeni ya kukomesha vitendo hivyo kwa kutoa elimu kwa jamii yenye lengo la kutambua viashiria vya ukatili huo.

> **Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WilDAF) na Mtandao wa Kupinga na Kupambana na Ukatili imekuwa ikifanya kampeni ya kukomesha vitendo hivyo .....**

Vitendo vya ukatili ambavyo vimekuwa vikijitokeza kwenye baadhi ya maeneo nchini, ni pamoja na ukeketaji, vipigo, ubakaji, ulawiti, utelekezwaji wa familia utupwaji wa watoto, rushwa ya ngono na vingine vingi.

Ukiangalia suala la ukeketaji, ni wazi bado kikwazo, kwani siku chache zilizopita tangu kumaliza kwa siku 16 za maadhimisho ya kupinga ukatili wa kijinsia zilizofikia kilele chake Desemba 10, mwaka jana, tayari kulikuwa na baadhi ya watoto waliokimbia kwao kukwepa kukeketwa.

Hayo yalithibitishwa na Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii, Kipunguni jijini Dar es Salaam, Seleman Bishagazi, kwamba kituo chake kilipokea watoto watatu wa waliokimbia toka kwao maeneo ya Kitunda wakihofia kufanyiwa ukatili huo.

Kwamba mwezi Desemba baadhi ya makabila yanayojihusisha na vitendo hivyo, huwa ni wa ukeketaji na kwamba watoto ambao wamepata elimu kuhusu madhara ya ukeketaji, hukimbia kuukwepa.

Kuna haja ya kuongeza kasi ya kutoa elimu badala ya kusubiri maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili ambazo inawezekana zisiwe na matokeo mazuri zaidi kuliko elimu ambayo ingetolewa kila mara.

Mila na desturi potofu ambazo zinaendelea kupewa uzito na baadhi ya jamii, zinaweza kutoweka iwapo kila mmoja wetu ataona umuhimu wa kuachana nazo hasa baada ya kuelimishwa kwa kina.

Aidha, kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia ingekuwa ni ajenda ya kudumu katika vikao vya Kamati ya Maendeleo ya Mkoa (RCC), Wilaya (DCC), Kata (WDC) na vijiji, lakini viongozi wa dini na wazee wa mila washirikishwe.

Si vibaya wadau mbalimbali wakajitiokeza kuunga mkono kampeni hizi kwa kuchangia rasilimali fedha, ili wananchi wengi zaidi wafikiwe na kuelimishwa, lakini kupatiwa msaada wa kisheria.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Wanasheria walikuwa wapi katika haya?



Pascal Mayalla

NAENDELEA na zile makala za Kwa Maslahi ya Taifa, kutetea haki za msingi za kikatiba za Watanzania ambazo zimeporwa. Serikali ikalitumia Bunge kutunga sheria batili, Mahakama Kuu ikatamka sheria hiyo ni batili, serikali ikapeleka Bungeni kwa hati ya dharura, mabadiliko ya katiba yakafanywa kiubatili, na batili hiyo ikaingizwa kwenye katiba kiubatili.

Wakati hayo yote yakifanyika, yalifanyika huku tukiwa na wanasheria serikalini, bungeni na mahakamani! Kama haya yote yalifanyika na washeria wapo, swali ni hivi kweli anzania tuna wanasheria?

Nchi yetu inaendeshwa kwa mujibu wa katiba, sheria, taratibu na kanuni, kwa kutumia mihimili mitatu ya katiba ambayo ni Serikali, Bunge na Mahakama. Kwenye medani za sheria, kazi ya Bunge ni kutunga sheria, kazi ya Mahakama ni kutafsiri sheria na kazi ya Serikali ni kutekeleza sheria.

Mihimili hii kila mmoja una nguvu na mamlaka inayojitegemea, hivyo haipaswi kuingiliana. Kwa Kiingereza inaitwa “independent powers” yaani Serikali itaheshimu uamuzi wa Bunge na Mahakama na kutoingilia. Bunge litaheshimu uamuzi wa serikali na mahakama na haitaingilia na mahakama itaheshimu uamuzi ya Bunge na serikali haitaingilia.

Kwa vile vyombo hivi vinaongozwa na watu ambao ni binadamu na wanaweza kufanya makosa, mihimili hii mitatu ikapewa kazi ya kila mhimili kuwa ni mlinzi na msimamizi wa mhimili mwingine. Kazi hii ya ulinzi na usimamizi wa mihimili inatumia kanuni inayoitwa kwa Kiingereza “the doctrine of checks and balance’.

Serikali inalisimamia Bunge na Mahakama kwa kuteua watendaji wakuu na kulipa fedha za uendeshaji. Bunge linaisimamia serikali kwa kuitungia sheria, kuipitishia bajeti na kuisimamia serikali na mahakama ya kuitungia sheria. Mahakama inalisimamia Bunge na serikali na kuzifuta sheria mbovu zitakazotungwa na Bunge na kutoa amri ambazo serikali ni lazima izitekeleze.

Serikali ikivuka mpaka wa mamlaka yake, mfano mkuu wa serikali akikiuka katiba, kama ilivyofanyika kwenye kuzuia mikutano ya siasa, Bunge lilipaswa kumwondoa Rais madarakani kwa kutumia Ibara ya 56. Au Mahakama kuipinga ile amri batili ya Rais kwa kuiondoa na lazima serikali itekeleze. Hivyo, serikali inasimamiwa na kulindwa na Bunge na Mahakama, Bunge linasimamiwa na serikali na mahakama na mahakama inasimamiwa na Bunge na serikali.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina misingi mikuu minne ya uhuru, haki, udugu na amani. Misingi hiyo yaweza tu kutekelezwa katika jamii yenye demokrasia ambayo serikali yake husimamiwa na Bunge lenye wajumbe waliochaguliwa na linalowawakilisha wananchi na pia yenye Mahakama huru zinazotekeleza wajibu wa kutoa haki bila woga wala upendeleo wowote, hivyo kuhakikisha haki zote za binadamu zinadumishwa na kulindwa na wajibu wa kila mtu unatekelezwa kwa uaminifu. Katiba hii imetungwa na Bunge maalum kwa niaba ya wananchi kwa madhumuni ya kujenga jamii kama hiyo na pia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Tanzania inaongozwa na serikali yenye kufuata misingi ya demokrasia.

Kwa mujibu wa katiba hii, kitu muhimu kabisa kwa taifa la Tanzania ni watu. Watanzania hawa ndio wenye katiba. Kwa maana hiyo, katiba ni mali ya Watanzania. Ni watu hawa Watanzania, walioweka misingi mikuu minne ya Katiba uhuru, haki, udugu na amani. Msingi mkuu wa kwanza wa katiba yetu ni uhuru, wa pili ni haki, hivyo vitu viwili vikuu vya Katiba yetu ni uhuru na haki.

Katiba hii imetoa haki mbalimbali kwa Watanzania. Haki kuu ni uhuru na haki. Katiba imeeleza wazi kuwa misingi hiyo yaweza tu kutekelezwa katika jamii yenye demokrasia ambayo serikali yake husimamiwa na Bunge lenye wajumbe waliochaguliwa na linalowawakilisha wananchi. Maana yake ni kwamba Bunge linapaswa kuwa na wajumbe waliochaguliwa na watu ambao ndio wawakilishi wa wananchi. Katiba haikusema vyama vya siasa ndivyo vitawachagulia wananchi wajumbe wa kukuwakilisha. Ni kina nani waliokuja kuamua ili mtu uchaguliwe kiongozi ni lazima udhaminiwe na chama cha siasa?

Katiba pia imetoa maelekezo mahususi kwenye mhimili wa Mahakama kwamba Mahakama lazima ziwe huru zinazotekeleza wajibu wa kutoa haki bila woga wala upendeleo wowote, hivyo kuhakikisha haki zote za binadamu zinadumishwa na kulindwa. Swali lile la wakati haki za msingi za Watanzania zilizotolewa na Katiba, ziliponyofolewa huku mahakama imepewa jukumu la kuhakikisha haki zote za binadamu zinadumishwa na kulindwa, ipo na inaangalia tu, mahakama zilikuwa na wanasheria kweli?

Kuna uamuzi fulani wa mahakama yetu unaosema “the court is not the custodian of the constitution”. Kama mahakama yetu inaweza kutoa uamuzi wa namna hii na huku Tanzania tuna wanasheria nguli na hawakufanya lolote, je, tuna wanasheria kweli?

Tukutane wiki ijayo kwa mwendelezo wa makala hii ili kuwafungua macho Watanzania wenzangu, tuone jinsi haki kuu mbili za kikatiba zilizotolewa na katiba yetu, jinsi zilivyokuja kuporwa huku wanasheria wakiwapo bila kufaya chochote. Pia tutayaendelea kumshukuru Mungu kwa ajili ya kutuletea Rais Samia Suluhu Hassan kwani siku anaruhusu mikutano ya vyama vya siasa, alifungua milango ya marekebisho ya sheria pamoja na marekebisho ya Katiba.

**Wasalaam.**
**Paskali**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Ni aibu kutelekeza kilimo ili kucheza kamari



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

WATANZANIA pengine hata watu wa mataifa mengine, tumekuwa tukiishi na kaulimbiu ya Kilimo ni Uti wa Mgongo kwa kuzingatia na kuamini, kuwa hakuna maisha bila chakula na chakula hakipatikani bila kilimo.

Na hiyo imetokana na ukweli kuwa tangu mwanzo wa maisha ya binadamu ulimwenguni, maisha yalitegemea ardhi kwa maana ya kupata chakula ardhini kitokanacho na majani, matunda, mbegu na mizizi.

Vyote hivyo pamoja na nyama, visingekuwapo kama ardhi inayozalisha mimea isingekuwapo. Kilimo kilikuja kama mbadala wa uokotaji na uchumaji matunda na uchimbaji mizizi, hasa baada ya kugunduliwa zana za chuma.

Binadamu alipogundua kuwa anaweza kutengeneza kifaa cha chuma chenye mpini akakiita jembe, ndipo alipoweza kutifua ardhi akapanda mbegu zikamea na hatimaye kuvuna chakula chake.

Hata mapinduzi ya viwanda yalipotamalaki duniani, bado binadamu hakuweza kutengeneza chakula bila kutegemea ardhi, hivyo alichokifanya kikawa ni kufanya mabadiliko katika zana za kilimo kuendana na wakati.

Nasi Watanzania hatujabaki nyuma katika kuamini kwenye kilimo na ndiyo sababu tumekuwa kila zama tukija na kaulimbiu za Siasa ni Kilimo, Kilimo ni Kazi, Kilimo cha Kisasa na hata Kilimo Kwanza na kauli zingine za kusajihisha kilimo.

Hata hivyo, jinsi zama zilivyokuwa zikibadilika, bado kilimo kiliendelea kuonekana si kazi yenye heshima na staha, zaidi ya kazi za ofisini zilizoendana na utanashati, kwani kilimo kilibaki kuwa kazi ya jasho na kuchafuka.

Kilimo kilibaki kuwa kazi ya masikini, hivyo kama ulikwenda shule na kubahatika kuhitimu darasa la nne au la nane, hukustahili kuwa mkulima, ila kukaa ofisini au darasani kufundisha.

Enzi hizo mavazi meupe yakiendana na soksi nyeupe yakivaliwa na walimu kuonesha usomi wao lakini utanashati uliotokana na kazi zao huku mkulima akivaa masulupwete, kuashiria kazi aliyoifanya ya kuchezea udongo mchana kutwa.

Lakini wote walioona kilimo si kazi ya staha, walitegemea chakula kutoka kwenye kilimo; Baniani mbaya kiatu chake dawa hakika! Lakini bado walikidharau na kubaki kuwa kazi yenye hadhi ya chini pengine kuliko zote.

Hata hivyo, bado asilimia kubwa ya Watanzania ni wakulima na ndio wanaoishi vijijini na kulisha mamilioni ya watu wa taifa hili, licha ya kuifanya kazi hiyo katika mazingira magumu yenye ardhi chovu kirutuba na zana duni.

Pamoja na hali hiyo, lakini miaka yote nchi imekuwa na wizara inayosimamia sekta hii muhimu pengine kuliko zote katika maisha na kila mara wizara imekuwa ikija na mikakati tofauti ya kuhakikisha kilimo kinakuwa na tija.

Hivi sasa dunia inapitia kipindi kigumu cha mabadiliko ya hali ya hewa au tabianchi, hali inayotishia usalama wa chakula na hata sisi hatuepuki hali hiyo ambayo imechangiwa na mambo mengi.

Uharibifu wa mazingira ndilo tatizo ongozi linalochangia hali hiyo na kutishia siku zijazo dunia kukumbwa na joto kali lakini na hewa ukaa na hivyo kuathiri uzalishaji wa chakula na bila hatua kuchukuliwa, hali itakuwa mbaya.

Wizara ya Kilimo chini ya Hussein Bashe, bahati nzuri imeligundua hilo na sasa kuchukua hatua ya kujihami, angalau hata kupunguza kama si kuzuia kabisa janga linaloinyemelea dunia. Endapo hatua hazitachuliwa, kuna hatari ya kilimo kudumaa na chakula kukosekana.

Wizara inachukua hatua nyingi, ikiwa ni pamoja na kushirikisha vijana ambao ni wengi na ndio nguvukazi ya taifa katika kuanzisha miradi ya kilimo kwa jina la Kilimo Biashara, ambapo vijana huchukuliwa na kupewa ardhi kwa ajili ya kilimo cha kisasa.

Hii ni hatua inayotakiwa kuchukuliwa na kila kijana Mtanzania mwenye maono chanya na maisha yake lakini na mustakabali chanya wa Taifa lake, hapa ina maana vijana wafungue macho na kuingia katika mradi huu muhimu.

Lakini katika kulitekeleza hili, nchi kwa maana ya viongozi, inatakiwa kuwa bega kwa bega na wizara hii ambayo kwa maoni yangu, ndiyo mama kwani ni mtambuka na kila aliye katika sekta nyingine hataishi bila hii.

Hili wimbi la kamari lililobuniwa hivi sasa na kuimbwa katika kila redio nchini, likisimamiwa na serikali sambamba na kubeti, kama vitaendelea kupapatikiwa na kula muda wa vijana, hatimaye hakuna kijana atakayeingia kwenye kilimo, bali kutegemea kipato duni cha kamari.

Itashangaza kama si kusikitisha, kuona kamari hizi zikipewa kipaumbele kwa vijana hawa wanapokaa wakisikiliza redio na kutumbukiza kidogo walichonacho, huku wapatao wakiwa wachache.

Aghalabu wengi sasa wanashinda na kukesha kwenye ofisi za kubeti wakisubiri kushinda, badala ya kutumia nguvu zao kuzalisha chakula. Serikali ifungue macho Bashe na wenzake waungwe mkono katika hili. Alamsiki!

## Alliance One yatoa vifaa tiba, kompyuta

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, amepokea vifaa vya operesheni ya mifupa pamoja na kompyuta tatu kutoka Kampuni ya Alliance One Tobacco ya mjini hapa, vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni nane, vitakavyosaidia upasuaji wa mifupa mirefu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo juzi, Msando aliishukuru kampuni hiyo kwa kuitikia ombi la changamoto ya kutokuwapo kabisa kwa vifaa vya aina hiyo hospitalini huko, hivyo kulazimika kupeleka wagongwa hospitali zingine ikiwamo ya Taifa Muhimbili.

"Kwa mfano niliambiwa kuwa hospitali hii ilikuwa na wagonjwa wapatao 98 wanaohitaji upasuaji wa namna hiyo na kati ya hao 56 ndiyo walipewa rufani kwenda Dar es Salaam, wengine walikuwa hapa hospitali wanataabika tu na wengine wakikimbilia kwenye tiba mbadala," alisema.

Kiongozi huyo alisema baada ya kuelezwa hilo na viongozi wa hospitali, ndipo aliwaandikia barua Kampuni ya Alliance One kuomba msaada huo na walilikubali ombi hilo pasipo kusita.

Alisema vifaa walivyopokea ni pamoja na kompyuta tatu ambazo zitapelekwa kwa Jeshi la Polisi ili kusaidia katika kuleta ufanisi wa kazi zao.

Katika hatua nyingine, Msando alitoa rai kwa waliopewa vifaa hivyo ambao ni Jeshi la Polisi na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro kuvitunza vizuri na kutumika kwa kazi iliyokusudiwa.

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Allance One, Blasius Lupenza, alisema msaada huo unakwenda sambamba na sera ya kampuni hiyo kwa jamii iliyojikita kwenye maeneo ya maji, elimu na afya, ambapo wamefanya mambo mengi kwa jamii ya Mogororo.

Akitoa mfano, alisema kipindi cha UVIKO-19, kampuni ilitoa vifaa mbalimbali katika taasisi mbalimbali za serikali ili jamii ijikinge na ugonjwa huo.

Aidha, alisema walikarabati magari ya polisi na kuyanunulia matairi, pia wanaendelea kutoa huduma kwa kadri wanapoombwa.

Msemaji Mkuu wa Kampuni hiyo, John Magoti, alisema kampuni yake inafanya hayo ili kuitikia wito wa serikali kuhakikisha wananchi wanapata huduma iliyo bora.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Daniel Nkungu, aliishukuru Allance One kwa kuwapa seti moja ya vifaa vya upasuaji wa mifupa mirefu na kuongeza kuwa vitasaidia kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufani kwenda hospitali zingine.

Alisema kabla ya kupokea seti hiyo, walikuwa wanakumbana na changamoto ya wagonjwa kusubiri ndani ya siku tatu mpaka wiki moja, ili kufanyiwa upasuaji na wakati mwingine wakiazima vifaa kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, ili kufanikisha malengo kwa wagonjwa.

Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Morogoro, Samson Cornel, aliwaasa madereva wa pikipiki na bajaji kuwa na nidhamu wawapo barabarani ili kupunguza ajali ambazo hazina ulazima.

Aliishukuru Alliance One kwa kuwasaidia vifaa vya kompyuta huku wakiahidi kuvitunza.



Mbunge wa Manonga, Seif Gulamali, akizungumza wakati akiwapongeza wanafunzi waliofaulu Mtihani wa Taifa wa kidato cha pili wa Shule ya Sekondari Ziba wilayani Igunga mkoani Tabora juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi, mwalimu wadaiwa kulipwa 600,000/- kumwachia mtuhumiwa

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WAZAZI wa mwanafunzi wa darasa la sita (jina la shule linahifadhiwa) wilayani Shinyanga pamoja na mwalimu wake, wanadaiwa kulipwa Sh. 600,000 ili kumwachia kijana anayedaiwa kumbaka mwanafuzi huyo.

Mwanafunzi huyo mwenye umri wa miaka 11 (jina linahifadhiwa) anadaiwa kufanyiwa ukatili huo Oktoba, mwaka jana, na baada ya kubainika kwa jambo hilo, wazazi wake na mwalimu wake wanadaiwa walilipwa kiasi hicho cha fedha ili kumaliza kesi hiyo.

Makubaliano hayo yalifanyika kwa wazazi wa pande mbili na inadaiwa kwamba wazazi wa mwanafunzi aliyebakwa walilipwa Sh.400,000 kati ya 600,000 zilizotolewa na wazazi wa mbakaji na Sh. 200,000 zililipwa kwa mwalimu huyo, aliyetajwa kuwa ni Roseline Kilekali. Ofisa Mtendaji wa Kata ya Pandagichiza Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Deogratius Mashamba, aliyabainisha hayo juzi alipozungumza na Nipashe kwa njia ya simu.

Alisema tukio hilo lilitokea mwezi Oktoba, mwaka jana, na kusuluhishwa kimyakimya na wazazi wa pande mbili bila uongozi wa serikali kufahamu.

Mashamba alisema, taarifa za tukio hilo alizipata baada ya raia wema kutoka katika kijiji cha Sayu, anapoishi mwanafunzi huyo, kutofurahishwa na kitendo kilichofanywa na wazazi hao, hivyo kutoa taarifa ofisini kwake.

Aliongeza kuwa kitendo hicho kimesababisha mwanafunzi huyo kuathirika kisaikolojia licha ya kuwa bado anaendelea na masomo.

Baada ya kuripotiwa tukio hilo, alisema alitoa taarifa katika vyombo vya sheria ili wahusika watafutwe na kuchukuliwa hatua na hivi sasa uchunguzi unafanywa na vyombo vya ulinzi likiwamo jeshi la polisi kwa kushirikiana na ofisi yake na serikali ya kijiji anachotoka.

Mwanafunzi anayedaiwa kubakwa, alisema siku ya tukio alikutana na kijana huyo aliyejulikana kwa jina moja la Ng'andu akiwa anachunga kondoo na alimwita lakini alikataa, hivyo kuamua kumkimbiza na alipomkamata alimvutia kichakani na kumwingilia kwa nguvu na kumsababishia maumivu makali.

"Ilikuwa nyakati za jioni wakati nimetumwa na wazazi mafuta ya kula dukani. Wakati narejea nyumbani nilikutana na Ng'andu akichunga kondoo wao.

Aliponiita nilikataa na kukimbia na alinikimbiza pale aliponishika alinivuta kichakani na kunibaka.

Nilipiga kelele lakini sikupata usaidizi mpaka nilipofika nyumbani na kutoa taarifa," alisema.

Baba mdogo wa binti huyo, Emmanuel Ntunze, alisema waliitwa shuleni anakosoma mwanafunzi kwa ajili ya kusuluhishwa na wao waliitikia wito na kikao kiliongozwa na mwalimu mkuu wa shule hiyo, Roseline Kilakali. Alisema katika kikao hicho, waliamua kumtoza faini ya Sh. 600, 000 kijana huyo na Sh. 400,000 walichukua wao na Sh. 200,000 zililipwa shuleni.

Kwa mujibu wa Ntunze, baada ya shule hiyo kupokea fedha hizo, binti aliruhusiwa kuendelea na masomo na kukiri kwamba hawakumpeleka hospitalini kwa ajili ya vipimo vya afya yake na kwamba walilazimika kufuata maelekezo ya viongozi wa shule na kulimaliza na hakuwa na uelewa nini wafanye baada ya tukio hilo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Sayu, Lucas Mpuya, alikiri kutokea kwa tukio hilo na halikufikishwa katika ofisi yake kwa ajili ya hatua zaidi ya kisheria badala yake taarifa alizipata kutoka kwa raia wema ambao hawakufurahishwa na kitendo cha wazazi wa pande zote cha kukubaliana kupeana fedha.

# Ufafanuzi ndege zinazotua katika hifadhi

**Na Maulid Mmbaga**

WIZARA ya Maliasili na Utalii, imesema ndege zinazotua na kuruka katika viwanja ndani ya hifadhi zinasafirisha watalii kutoka Uwanja wa Ndege Dar es Salaam (JNIA), Kilimanjaro (KIA) na Abeid Amani Karume, Zanzibar.

Ufafanuzi huo unatokana na taarifa zilizosambaa kupitia mitandao ya kijamii kuwa ndege zinazoruka na kutua katika maeneo ya hifadhi zinasafirisha wanyamapori na rasilimali nyingine zinazolindwa na kuhifadhiwa kisheria.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na kitengo cha mawasiliano cha wizara hiyo, taarifa hizo sio za kweli na wanawaomba wananchi kuzipuuza, kwa kuwa zina nia ovu ya kusababisha taharuki katika jamii.

"Tanzania ni nchi iliyobarikiwa vivutio vingi vya utalii zikiwamo hifadhi za taifa 22, mapori ya akiba 22, mapori tengefu 29, Hifadhi ya Ngorongoro, hifadhi za misitu, maeneo ya kihistoria na urithi wa dunia, hifadhi za bahari na fukwe, maziwa makuu, mito na maeneo mengine mengi ya asili.

"Maeneo haya ya vivutio yamekuwa yakitembelewa na watalii wa aina mbalimbali na kuliingizia taifa fedha za kigeni pamoja na kuzalisha fursa za ajira," ilisema.

Taarifa hiyo iliendelea kufafanua kuwa watalii wengi wanatembelea Tanzania kutokana na juhudi kubwa za kutangaza utalii zilizofanyika ambazo zimekuwa kichocheo cha shughuli mbalimbali zikiwamo za utalii wa picha, safari za parachute, kutembea nyikani, ufukweni na kupanda milima.

Aidha, ilieleza kutokana na umuhimu wa shughuli hizo, serikali imefanya maboresho ya kukarabati miundombinu ya utalii vikiwamo viwanja vya ndege, barabara na miundombinu mingine muhimu katika maeneo ya hifadhi, ili kuwezesha uendelevu wa shughuli za uhifadhi.

Wizara imewahakikishia Watanzania kuwa viwanja vyote vya ndege katika maeneo ya hifadhi viko salama na vinatumika kwa shughuli za usafirishaji wa watalii wanaotoka katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

"Wizara iko makini kuhakikisha matumizi sahihi ya viwanja hivyo kwa wageni wote wanaoingia na kutoka katika maeneo ya hifadhi.

Tunawaomba wananchi muwe watulivu na kuwa makini na watu wanaotoa taarifa za upotoshaji na za kichochezi zisizo rasmi kuhusu ndege na matumizi ya viwanja hivyo," ilisisitiza.

Pia wizara iliwasisitiza wananchi wanapoona matumizi yasiyo sahihi wasisite kutoa taarifa kwenye vituo vyao vya uhifadhi, polisi au ofisi za serikali zilizo katika maeneo yao, ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za taifa.

# MAISHA

JANUARI 15, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 13

**Sheria za suti**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Hizi ni faida za sofa za ngozi



Ukurasa 12

**BIRTHDAY**




# Viganja vinavyobeba urembo

Ukurasa 14

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | D | U | N | D | A |
| ■ | U | ■ | ■ | E | ■ |
| U | M | A | ■ | R | ■ |
| ■ | A | ■ | B | E | I |
| ■ | Z | ■ | ■ | V | ■ |
| W | A | N | G | A | ■ |

## AMSHA AKILI


HAYA, TAFUTA NJIA YA KUMKAMATA SUNGURA MJANJA




## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
IGA, UMA, JANGA, JEMBE, BONGEA, JAMBIA

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MWALIMU mkuu alitembelewa na wanafunzi wageni shuleni kwake, aliwakaribisha katika viti.

Mwalimu: Kaeni kwenye nianze kuwauliza baadhi ya masomo

Mwanafunzi: Lakini mwalimu tumekuja hapa kutembelea shule na si kuulizwa.

Mwalimu: Kwani kuna tatizo kuwauliza watoto wangu?

Mwanafunzi: kabla ya kuja hapa tumeambiwa tusiseme chochote.

**SWALI**

Makaa yam awe yanapatikana wapi hapa Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Dalili za watu wanaoteswa na roho mbaya za mizimu!

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada yetu ya wiki iliyopita kuhusu roho zinazorudisha watu kuwa wa zamani. Yaani wanafanya vitu vile vile hawaonyeshi mabadiliko.***

Wiki iliyopita nilijadili sana kuhusu roho ya mizimu inavyotesa wengi pasipo wao kujua. Nikasema, kwa mfano, wanawake wengi sana wanateseka kwenye ndoa zao kwa sababu ya mizimu inayotawala koo/familia zao.

Ni muhimu unapogundua kuwa yapo mambo mabaya yanakutokea katika maisha yako, hata kama umefanya bidii ya kutosha kuyatatua, ni muhimu uingie rohoni na kuchunguza misingi yako. Yamkini unahitaji kutoka katika vifungo vya roho hii ya mizimu, hivyo unalazimika kuchukua likizo kwa wiki kadhaa ufunguliwe, zikuachie.

Mtu atauliza ni kwa nini uchukue likizo? Hiyo ni kwa sababu roho hizi zinaweza kuwa zimekaa kwenye ukoo wenu kwa muda wa zaidi ya miaka kumi, hivyo maombi ya siku moja tu hayatasaidia.

Maana hii mizimu imetambikiwa kwa miaka mingi na maagano yaliyowekwa ni makubwa sana. Kama hukuyashughulikia na kuyaua kabisa, yanaweza kulipiza kisasi na kukuangamiza.

> **"Nani huyo mtoto aliyezaliwa? Huyu ni Musa na ndipo matatizo yake yalipoanzia. Musa aliishi maisha ya ajabu sana na ya tofauti sana. Alikuwa ni mtoto wa mfalme wa Misri.**

Maombi yanasisitizwa kwa sababu hili ni jambo zito na kama watu wakifunguliwa, watakuwa na upenyo mkubwa katika maisha yao na nchi zao.

Tukiangalia kwenye maandiko ya Mungu, zipo roho zilizowafuatilia watumishi wa Mungu, Musa akiwa mmoja wao. "Simeoni na Lawi ni ndugu; panga zao ni silaha za jeuri. Nafsi yangu usiingie katika siri yao, fahari yangu usiungane na kusanyiko lao, maana katika ghadhabu yao walimuua mtu, na ukaidi wao walikata mshipa wa ng'ombe. Ghadhabu yao na ilaaniwe, maana ilikuwa kali na hasira yao maana ilikuwa haina huruma. Nitawagawa katika Yakobo, nitawatawanya katika Israel (Mwanzo 49:5-7).

Hapa tunaona mambo mawili yaliyokuwa yakikaa ndani ya Simeoni na Lawi; Ghadhabu na hasira ambayo iliwafanya waue mtu.

Tuangalie tena mfano huu; Mtoto mmoja katika nyumba ya Lawi akaondoka akaoa binti mmoja wa Lawi. Yule mwanamke akachukua mimba akazaa mwana na alipoona ni mtoto mzuri akamficha miezi mitatu.

Kutokana na laani iliyokuwa ikimfuatilia Lawi, tunaweza kusoma andiko hili; "Mtu mmoja katika nyumba ya ghadhabu na hasira akaondoka akaoa binti mmoja wa ghadhabu na hasira. Ina maana ndoa hii tayari ilikuwa inawakilishwa na ghadhabu na hasira". (Kutoka 2:1-2).

Nani huyo mtoto aliyezaliwa? Huyu ni Musa na ndipo matatizo yake yalipoanzia. Musa aliishi maisha ya ajabu sana na ya tofauti sana. Alikuwa ni mtoto wa mfalme wa Misri. Alikuwa mtu wa kutoa sheria.

Alikuwa ni mtumishi mwaminifu sana mbele za Mungu, na mpole kuliko mwanadamu yeyote aliyewahi kuishi. Musa aliona uso wa Mungu. Alikuwa akipewa ujumbe na Mungu kuwafikishia watu. Alikuwa ni mnenaji wa Mungu, mwimbaji na nabii wa kipekee sana. Alikuwa ni mtoto wa mtumwa lakini aliishi kwenye nyumba ya mfalme.

Musa alikuwa na kigugumizi na mwanadamu, lakini alipokuwa anaongea na Mungu aliongea moja kwa moja bila kigugumizi. Alikuwa ni shujaa wa ajabu, alikufa peke yake mlimani na alizikwa na Mungu mwenyewe. Unaweza kuona sifa alizokuwa nazo Musa, lakini ile roho ya ukoo ilikuwa inamfuatilia, hivyo kujikuta anaua.

Andiko hili linabainisha hilo. "Hata siku zile Musa alipokuwa mtu mzima...alimwona mmisri anampiga Mwebrania, mmojawapo wa ndugu zake. Basi akatazama huko na huko, na alipoona hapana mtu akampiga Mmisri yule, akamficha ndani ya mchanga.

"Akatoka siku ya pili, na tazama watu wawili Waebrania walikuwa wakipigana. Akamwambia yule aliyemdhulumu mwenzake, mbona unampiga mwenzako? Yule akasema, ni nani aliyekuweka wewe kuwa mkuu wetu? Je, unataka kuniua mimi kama ulivyomuua yule Mmisri? Musa akaogopa, akasema, Kumbe! Jambo lile limejulikana"(Kutoka 2:11-14).

Msomaji wangu, sasa nimalizie mada yetu kwa kukumegea baadhi ya dalili kumjua mtu anayefuatiliwa na roho za mizimu. Huota ndoto za watu waliokufa, hakui kiroho, umasikini uliokithiri, kushindwa tu pale anapokaribia upenyo.

***Dalili zingine anafuatiliwa sana na roho za kiganga, ni mtu asiyejipenda (ni mchafu). Kama ni mwanamke anakuwa na roho za kiume, mafarakano kwenye ndoa na ndoa za wake wengi. Je, una kisa? Ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Ubakaji, ulawiti unaongezeka jamii tuchukue hatua

KILA uchao, suala la ubakaji na ulawiti limekuwa likizungumzwa na kuripotiwa katika vyombo vya habari hali inayoonyesha kuwa tatizo hilo linazidi kuota mizizi. Kesi nyingi zinaelezwa kuishia polisi au mtuhumiwa anapopewa dhamana familia zinakaa kuzungumza ili kuyamaliza kifamilia.

Aidha, baadhi ya vijana waendesha bodaboda wanadaiwa kuhusika na matukio hayo hasa wale wanaowabeba wanafunzi kuwapeleka shule, kiasi kwamba wako watoto wamefanyiwa ukatili na kuzoea au kulazimishwa kuishi maisha ya mateso tangu wakiwa wadogo.

Kwenye shule za msingi na sekondari, matukio hayo yanaongezeka kwa watoto kufanyiwa hivyo na ndugu wa karibu, ambao hulala nao wanapokaribisha na mama, baba au mlezi anashtuka mtoto ameshaharibika.

Aidha, inadaiwa fedha inatumika kumaliza kesi hizo na wakati mwingine madawati ya jinsia yamelalamikiwa kuwa sehemu ya uharibifu, ambao sasa ni maumivu kwa jamii.

Unapokwenda maeneo ya starehe utakutana na vijana wa kiume wa rika mbalimbali wanajiuza yaani wanaingiliwa kinyume cha maadili na wanaume wenzao, huku wasichana wakiwa na mahusiano na wasichana au wanawake wenzao.

Vitendo hivi vinaua kizazi kwa kuwa idadi ya wanaume inaendelea kupungua kila siku, huku takwimu zilizoko zikonyesha wanaume ni wachache ikilinganishwa na wanawake, sasa linapotokea suala la ulawiti linapunguza idadi yao na kukiweka kizazi hatarini.

Inaelezwa kuwa mwanamume anapofanyiwa kitendo hicho, anatamani kuendelea kufanyiwa ndiyo maana wengi hujiuza ili kupata wa kuwafanyia hivyo, hii ni kosa kisheria na limekatazwa na kulaaniwa kwenye vitabu vitakatifu vya dini.

Utafiti mdogo uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Mshataka, ulibaini kuwa baadhi ya watuhumiwa wa makosa hayo wakiwa nje kwa dhamana wanakimbia na wengine kuharibu ushahidi au kumalizana na wazazi ama ndugu wa mhanga wa vitendo hivyo.

Aidha, Kaimu Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za Sheria kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Happy Msimbe, hivi karibuni alisema serikali imeanza mchakato wa kufanyia marekebisho Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na wanaanza mchakato wa makosa ya ubakaji na ulawiti kuondolewa dhamana.

Baadhi ya familia zinamaliza kesi hiyo nyumbani, inapotokea mzazi mmoja anashikilia kuendelea na kesi mahakamani anaitwa na kukalishwa na ukoo, ikiwamo kutengwa kama atakubali kuendelea na kesi.

Wengi wanaokumbwa na kesi hizi wanatoka familia maskini ambazo wakati mwingine kufuatilia kesi ni usumbufu na gharama, wakati mwingine wanakutana na usumbufu mkubwa polisi na hospitali na kuamua kubaki nalo moyoni.

Wanaoteseka ni watoto na wazazi wao ambao wametendewa ukatili huo, lakini hawana pa kukimbilia kwa kuwa kila eneo hakuna msaada na mwisho matukio kuendelea kutokea.

Mabadiliko ya sheria hiyo kuongeza makali ni hatua nzuri sana kwa kuwa watu wataogopa na kesi zitashughulikiwa inavyotakiwa kwa kuwa ushahidi hautaharibiwa kama inavyofanyika sasa.

Ni muhimu kulinda taifa dhidi ya ongezeko la mashoga ambao wanakuwa hivyo siyo kwa msukumo wa maumbile, bali kwa kufanyiwa ukatili na wachache ambao wananufaika au ni tamaa za mwili.

Lakini ni muhimu kuendelea kutoa elimu na kuchukua hatua mapema taarifa zinapotolewa, kuboresha madawati ya jinsia ili yasiwe kichaka cha rushwa na kuumiza watu, viongozi wa dini walio waadilifu kuendelea kuwahubiri yaliyomema waumini wao na kuwaonya kwa kutumia maandiko matakatifu juu ya vitendo hivyo.

Sheria kufanyiwa mabadiliko ni jambo jema, lakini bila kudhibiti rushwa ni sawa na bure kwa kuwa watu wataendelea kufinyanga kesi za namna hiyo, ili kupata fedha kwa waliotenda pasipo kuona uharibifu huo ipo siku utabisha hodi kwenye nyumba yake.

Kwa sasa tuna Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Watoto na Makundi Maalum, ambayo imeunda kamati mbalimbali kukabili vitendo vya ukatili. Lakini ni muhimu kufuatilia hadi ngazi ya chini hasa kwenye shule za msingi na sekondari, lakini kuimarisha idara ya ustawi wa jamii, polisi na hospitali ili wafanye kazi kwa hofu ya Mungu na kuogopa kuyaharibu matukio hayo.

Lazima jamii iwe wazi kwa kusema hapana kwa vitendo ukatili ambao unaelekea kuwa jambo la kawaida sana, mifumo ifanye kazi vyema, kamati za kupinga ukatili kuanzia ngazi ya mtaa zitekeleze wajibu wake.

# SHEREHE YA KUZALIWA







Desemba 31, 2022 ilikuwa siku ya furaha kwa mtoto Precious Samwel baada ya kusherehekea kumbukizi ya kuzaliwa kwake akiwa na familia yake katika Hoteli Verde ya Zanzibar.







MITINDO







# Sheria za suti

JE, unafahamu sheria au kanuni za kuvaa suti? Kama unapenda kuvaa vazi hili na kwamba hujui kanuni za jinsi ya kuvaa suti, basi fahamu kuna utaratibu maalumu wa kutumia vazi hilo.

Kuvaa suti na umaridadi ni muhimu kuchagua suti ya saizi yako, inayokutosha na unahisi vizuri, lakini ni muhimu sana kuchagua mavazi mengine ambayo utavaa ili kukamilisha vazi.

Pia unatakiwa kujua jinsi ya kufunga suti, kwa sababu hata tukivaa suti nzuri, ya bei ghali na kushonwa na fundi cherehani bora ulimwenguni, unaweza kuharibu kila kitu ikiwa hatujui jinsi ya kufunga suti.

Ikiwa hauvai suti mara nyingi na haujui kuifunga au kwa urahisi na licha ya ukweli kwamba unavaa kila siku, haujawahi kujua jinsi ya kufunga, usijali kwa sababu katika makala hii yote utajifunza jinsi ya kuifanya.

**Koti la kifungo kimoja**

Ili suti yako ikamilike lazima uwe na koti juu, aina rahisi ni koti la kifungo kimoja au wengine wanaita 'bleza'.

Koti la aina hii hulazimiki kufikiria kama unataka kuifunga au la.

Unachopaswa kufanya ni wakati wote unaposimama lazima ufunge kifungo cha koti lako na unatakiwa kufungua vifungo wakati unakaa chini.

**Koti la vifungo viwili**

Koti ya vifungo viwili linatumiwa karibu na wanaume wote. Ikiwa unataka kuwa na vifungo kwa njia inayofaa, kumbuka wakati umesimama lazima uwe umefunga kifungo cha juu pekee.

Kumbuka, unapotaka kukaa vifungo vya koti kilifungwa, sharti kifunguliwe ili kuepuka mwonekano mbaya.

**Koti la vifungo vitatu**

Suti zenye vifungo vitatu au vinne zinahitaji kufikiria kidogo juu ya kifungo gani cha kufunga. Mapendekezo bila shaka ni kufunga kifungo cha kati wakati unaposimama.

Haupaswi kamwe kufunga kifungo cha chini au cha juu.

Ikiwa koti lina vifungo 4 unapaswa kufunga vifungo viwili vya katikati na ikiwa inakufaa au basi funga cha juu kabisa.

Kama ilivyo katika kesi zilizopita wakati wa kukaa chini, unaweza kufungua vifungo vyote au kuacha cha chini kimefungwa, ingawa ni bora kuiacha imefunguliwa ili kukupa mwonekano wa kupendeza.

UREMBO









# Viganja vinavyobeba urembo

MIKONO, viganja na vidole ni kati ya sehemu muhimu katika mwili wa mwanamke.

Mikono hutumika kufanya shughuli nyingi za nyumbani na sehemu mbalimbali katika maisha kuanzia kutandika kitanda, kupika, kufanya usafi, kuandika, kujiremba pamoja na majukumu mengine mengi.

Mikono isipotunzwa vizuri ni rahisi sana kuharibika, kupoteza mvuto wake wa asili na kuharibu afya ya kucha.

Hitaji la urembo wakati mwingine humsukuma msichana katika matumizi ya vipodozi vya kupaka kwenye kucha zake ili kukamilisha urembo wake.

**Epuka kufanya haya**

Kwa ajili ya afya bora ya viganja na kucha, anashauriwa kula mboga za majani, maharage, korosho, asali na matunda kwa wingi kila siku.

Usafi wa kucha kila siku kwa kuziosha kwa maji ya uvuguvugu na sabuni laini pamoja na brashi ndogo ya mikono huimarisha afya.

Kucha pia zinaweza kusafishwa kwa maji ya mmea wa mshubiri (Aloevera), kitunguu saumu kilichopondwa pondwa au kitunguu maji kisha viganja na vidole vikaushwe vizuri na kupaka losheni.

Kucha zinatakiwa zisiwe ndefu ili kuepuka utunzaji wa vimelea vinavyosababisha magonjwa na kurahisisha utunzaji na usafi wa kucha.

Ni vizuri kulainisha ncha za kucha baada ya kuzikata kwa kutumia tupa ya kucha na kuzisugua kuelekea upande mmoja ili kuepuka kucha zisiwe kali na kurarua viganya wakati unapojikuna na kuvunjika.

Kusugua kucha kwa kwenda mbele na nyuma kunaweza kusababisha kucha zivunjike kwa urahisi na haraka.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Furahia juisi ya ukwaju

UKWAJU ni tunda lenye faida nyingi kwa afya ya mwanadamu.

Tunda hili linaliwa lenyewe au huweza kutumika kutengeneza juisi tamu.

Namna ya kutengeneza

Andaa maji kwenye beseni na uoshe kidogo ukimaliza chukua ukwaju wako weka kwenye sufuria yenye maji ya saizi na injika jikoni uache uchemke kwa dakika 10 hadi 15 ili uuwe vijidudu.

Dakika zikifika epua ukwaju wako na uache kwa muda upoe, andaa maji yako masafi na chujio ili uweze kuchuja juisi yako kwa uangalifu zaidi.

Kisha weka sukari kwa kiasi unachopendelea, pia ili kupunguza ukali na kuweka harufu nzuri unaweza kuunga kwa hiliki au vanilla.



Ukimaliza hapo, weka juice yako kwenye friji ili ipoe tayari kwa kunywa.

Faida ya ukwaju

Ukwaji ni chanzo kizuri cha viuasumu mwilini 'antioxidants' ambavyo huzuia saratani.

Husaidia kushusha joto la mwili na kuondosha homa, hasa homa ya malaria, homa ya matumbo na ni chanzo cha Vitamini B na C.

Juisi ya ukwaji husaidia kulinda mwili dhidi ya mafua na kero za mafua kooni na inasaidia mmengenyo wa chakula tumboni.

MAISHA NI NYUMBA
Na Elizabeth Zaya

# Hizi ni faida za sofa za ngozi



WATU wengi wanapenda kupamba nyumba zao kwa sofa za vitambaa kutokana na urahisi na zina machaguo mengi ya rangi.

Hata hivyo sofa za ngozi zina faida nyingi endapo utaweka ndani ya sebule kwa ajili ya kuipamba nyumba na kuwa sehemu safi ya kukaa.

Zifuatazo ni sababu tano za kuwa na sofa za ngozi ndani ya nyumba.

**Ubora**

Sofa za ngozi ni bora kwa kiwango cha juu na inaonyesha ufahari. Utengenezaji wa mtindo wa kisasa wa sofa za ngozi unazifanya kuwa maridadi zaidi.

**KUPAUKA**

Tofauti na sofa za vitambaa, aina ya ngozi kadri zinavyozidi kuzeeka, ndivyo ngozi yake inavyozidi kuwa laini na kukupa burudiko zaidi.

**Uimara**

Wataalamu wanakadiria kuwa sofa za ngozi zinaweza kudumu mara nne zaidi ya zile za kitambaa. Ngozi ni ngumu lakini ni laini inayovumilia hali ya hewa.

**Gharama**

Ni kweli sofa ya ngozi ina gharama, lakini ni vizuri kujua kuwa inadumu mara dufu na hivyo kukupunguzia gharama ya kubadilisha sofa kila wakati.





# Kifanye kitanda kama pambo la nyumba

USAFI wa kitanda ni jambo muhimu ambalo linapaswa kufanywa kila siku katika nyumba.

Pia usafi huo unaweza ukafanywa muda wowote ndani ya siku hiyo moja kwa kutegemeana na matumizi yake ili mradi kionekane kisafi wakati wote na unatakiwa uanze nyakati za asubuhi unapoamka hadi unapolala tena.

Na usafi ninaouzungumzia hapa ni kuanzia kutandika mashuka, kufuta vumbi katika pande zote zinazokizunguka na kukipangilia vizuri.

Kwa sababu kitanda ni moja ya vitu vinavyofurahisha nafsi kwenye nyumba na kiafya, pia ni vizuri kikapewa kipaumbele kikubwa.

Ni vizuri kukumbuka kuwa usafi wa kitanda si lazima uhitaji gharama kubwa. Ni jambo la kujipanga tu kujizoesha na kama ilivyo katika usafi wa vitu vingine. Kitanda pia kisipotunzwa vizuri hakiwezi kuwa bora na imara.

Kitu cha muhimu ni kuhakikisha unakuwa na shuka lako unalotumia kulalia pamoja na lile unalojifunika ambalo utalitumia pia katika shughuli hiyo ya kutandika. Endapo utaona inafaa zaidi kulingana na uwezo wako, tenga mashuka maalum ya kutumia wakati wa kulala na ya kutandika.

Ziko njia nyingi za kutandika kitanda na mojawapo ni kutandika katika godoro kwa kuhakikisha shuka limechomekwa ndani kabisa na la pili ukalitandika juu yake na kulikunja kidogo kwa robo ya kitanda au nusu kutoka juu unapoweka kichwa chako kwa kulishusha kwa chini.

Shuka hilo la pili ukiona inafaa likunjie kwa ndani ya godoro au kuliacha kwa nje.

Upande wa chini unapoelekeza miguu wakati wa kulala, weka hata shuka zito ambalo ikiwezekana liwe linafanana na mito yako ili kuongeza mvuto zaidi.






Lakini kumbuka kwamba usafi katika kitanda chako si lazima uwe na mashuka mengi isipokuwa tu kwa anayehitaji 'kukirembesha' zaidi, kama hauna mengi tumia hilo moja ilimradi liwe safi na mito yako kwa kulitandika kwa ustadi mkubwa.

Kwa sababu utandikaji wa kitanda ni usafi muhimu, pia usisahau kupangilia vizuri mito yako ili kukamilisha usafi zaidi wa kitanda chako na kukipendezesha, jifunze kubadilisha mpangilio wa mito, usipende kutumia wa aina moja.


Kumbuka kila kitu kinahitaji ubunifu, jitahidi kuongeza ubunifu kila siku kutafuta namna bora ya kukifanya kitanda chako kipendeze kwa sababu lengo kubwa ni kuipendezesha nyumba yako, nafsi na ustawi wa afya yako pia.


# KATUNI











***KINYUNYIZO CHA LEO...** ...HATA MCHELE UNA CHENGA LAKINI HAUWEZI KUFUNGA GOLI

HABARI KIMATAIFA

# Rais Biden azidi kubanwa kukutwa nyaraka za siri

**WASHINGTON,** MAREKANI

HALI inazidi kuwa tete kwa Rais wa Marekani, Joe Biden, baada ya nakala zinazoainishwa kuwa zilipatikana katika ofisi binafsi kuripotiwa kuwa ni pamoja na baadhi zilizowekwa alama za siri kuu.

Karatasi zilizo katika kiwango cha juu zaidi cha uainishaji zilikuwa kati ya faili 10 zenye jina lake, kwa mujibu wa mshirika wa BBC wa Marekani, shirika la utangazaji la CBS News.

Nyaraka zisizozidi 10 zilizoainishwa zilipatikana katika moja ya nyumba zake za Delaware, lakini hakuna zilizokuwa za siri kuu, ilisema CBS.

Kuvuja kwa habari ya juu ya siri kunaweza kusababisha athari kwa kiongozi huyo.

Kuna viwango vitatu vya msingi vya uainishaji wa Marekani, ikiwa suala kuwa la binafsi, siri na siri kuu.

Kwa ujumla, takriban faili 20 zilizoainishwa zilipatikana kati ya maeneo hayo mawili, inaripoti CBS, ikitoa mfano wa ofisa wa kutekeleza sheria katika shirikisho linalofahamu uchunguzi huo. Majarida hayo yalianza kubainishwa katika ripoti za habari ya Jumatatu iliyopita, lakini kundi la kwanza lilipatikana katika taasisi ya zamani ya Biden, Penn Biden Center huko Washington DC, mnamo Novemba.

Hiyo ilikuwa siku chache kabla ya uchaguzi wa katikati wa muhula, ambao ulishuhudia Republican wakishinda udhibiti wa Baraza la Wawakilishi la Marekani.

**BBC**



Wakulima wakijaribu kuondoa tope kwenye mfumo wa umwagiliaji katika shamba lao baada ya kimbunga kilichoambatana na mvua kubwa kulikumba eneo la Salinas, California, nchini Marekani, juzi. **PICHA: GETTY IMAGES**

# Iran yamnyonga waziri kwa ujasusi

**TEHRAN,** IRAN

HATIMAYE waziri wa zamani wa Iran ambaye ana uraia pacha wa Uingereza, Alireza Akbari, amenyongwa baada kupatikana na hatia ya ujasusi.

Familia ya Akbari ilikuwa imeombwa kwenda katika gereza lake kumwona kwa mara ya mwisho Jumatano na mkewe alisema alikuwa amehamishwa hadi katika gereza la peke yake.

Akbari alikuwa naibu waziri wa ulinzi wa Iran alikamatwa mwaka 2019 na kukutwa na hatia ya kufanya ujasusi kwa ajili ya Uingereza, jambo ambalo alilikanusha kuhusika.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Rishi Sunak, alisema kunyongwa kwake ni kitendo cha kinyama na kinaonesha udhaifu wa utawala mbaya.

"Mamlaka ya Iran hawakuwa na heshima za haki za binadamu za watu wa kwao wenyewe," alisema Sunak.

Aliongeza kwa kutoa salamu za rambirambi kwa marafiki na familia ya Alireza.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza, James Cleverly, alisema hukumu hiyo lazima ipingwe.

Chombo rasmi cha habari cha mahakama ya Iran, Mizan kiliripoti jana kuwa Alireza Akbari alinyongwa, bila kutaja tarehe ya kunyongwa kwake.

Habari hizo zilikuja baada ya Iran kuchapisha video ya Akbari mapema wiki hii ikionesha kile kilichoonekana kukiri makosa na baada ya wizara ya intelijensia wa nchi hiyo kumtaja raia mwenye uraia pacha wa Uingereza na Iran kuwa ni mmoja wa wahusika muhimu wa idara ya ujasusi ya Uingereza nchini Iran.

Katika ujumbe wa sauti alioutoa Akbari, alisema kuwa alikuwa akiishi nje ya nchi miaka michache iliyopita alipoalikwa kuja Iran kwa ombi la mwanadiplomasia mkuu wa Iran ambaye alihusika katika mazungumzo ya nyuklia na mataifa yenye nguvu duniani.



Waziri wa zamani wa Iran, Ali Reza Akbari.

Akiwa huko, alishutumiwa kupata taarifa za siri kutoka kwa katibu wa Baraza Kuu la Usalama la Taifa la Iran, Ali Shamkhani.

Akbari alidai kuwa alihojiwa na kuteswa na maofisa wa ujasusi kwa zaidi ya saa 3,500.

**BBC**

## Prince Harry: Ningesema yote nisingesamehewa na familia

**LONDON,** UINGEREZA

MWANAMFALME wa Uingereza, Harry amedai kwamba alikuwa na maelezo ya kutosha katika vitabu viwili, lakini alihofia kujumuisha baadhi ya vitu kwa sababu baba yake na kaka yake wasingeweza kumsamehe kamwe.

Aliiambia Daily Telegraph kuwa kuna baadhi ya mambo hakutaka kuyafichua ili ulimwengu kujua kinachoendelea ndani ya familia hiyo ya kifalme.

Pia alisema anataka kumuomba radhi mke wake Meghan kutokana na alichofanyiwa na familia yake.

Kitabu chake alichokiita 'Spare', kilichapishwa wiki hii, kimevunja rekodi kwa kuuzwa kwa kasi zaidi kuwahi kutokea nchini Uingereza.

Kitabu hicho kinaangazia orodha ndefu ya malalamiko dhidi ya Familia ya Kifalme, pamoja na msongo mkubwa wa mawazo tangu kifo cha mama yake, shida zake za afya ya akili, maisha ya kutengwa ambayo aliishi kabla ya kukutana na Meghan na kuvunjika kwa uhusiano wake na familia yake.

Kasri ya Kensington na Buckingham zote zimesema hazitatoa maoni juu ya yaliyomo katika kitabu hicho.

Katika mahojiano na Bryony Gordon wa Telegraph, ambaye alisafiri hadi California kuzungumza naye, Duke wa Sussex alisema kuwa hakuwa akijaribu kuangusha ufalme, lakini alijaribu kuwaokoa kutoka kwao wenyewe.

Prince Harry alisema kuna taarifa ambayo alimjulisha mwandishi wake JP Moehringer kwa muktadha huo, lakini hakukuwa na njia inayoweza kujumuishwa kwenye kitabu.

"Vingeweza kuwa hata vitabu viwili," alisema, akiongeza kuwa rasimu ya kwanza ilikuwa na kurasa 800, mara mbili ya nakala ya mwisho ya kurasa 400.

"kulikuwa na sehemu zingine ambazo nilimshirikisha JR, ambazo nilisema angalia tu, ninakuambia hii ni kwa muktadha lakini hakuna namna ambayo unaweza kuziweka taarifa hizo," alisema Prinxe Harry.

Alisema haiwezekani kusimulia hadithi yake bila wanafamilia wake ndani yake, kwa sababu wanachukua sehemu muhimu sana ya maisha yake na pia kwa sababu unaelewa wahusika na haiba ya kila mtu ndani ya kitabu hicho.

"Lakini kuna baadhi ya mambo yametokea hasa kati yangu na kaka yangu na kwa kiasi fulani kati yangu na baba sipendi tu ulimwengu uyajue maana sidhani kama watanisamehe," alisema.

**BBC**

MAKALA

# ZINGATIA MAMBO HAYA UNAPOTAKA KUANZISHA NA KUFANYA BIASHARA



Na Magabilo Masambu

LEO katika safu yetu hii tuzungumze kidogo kuhusu biashara. Kwa kiasi kikubwa, biashara ni maisha, kwa kuwa maisha hayajakamilika bila kuuza na kununua. Lakini zaidi, wataalamu wa fedha wanasema kama hauuzi chochote basi hatua za kuelekea kwenye mafanikio utakuwa unazisikia tu kwa majirani.

Kwanza, tutakubaliana kwamba biashara yoyote huwa inaanza na wazo lakini wazo bora lazima liwe limekusudia kutatua changamoto katika jamii. Mfano umepata wazo la kuuza maji maana yake unatakiwa kujua kama hilo ni tatizo katika eneo hilo.

Kwa hiyo jambo la kwanza kabisa unapotaka kuanzisha biashara, unatakiwa kufanya utafiti au uchunguzi mdogo kuhusiana na wazo lako la biashara. Utafiti huo utakuwa juu ya kutaka kufahamu changamoto kubwa waliyo nayo wananchi wa eneo hilo. Ikiwa utaanzisha biashara yako ni kwa kiasi gani utakwenda kutatua changamoto hiyo.

Biashara yoyote ambayo haiendi kutatua changamoto ya wakazi husika hata kama ungeifanya kwa miaka 100, hakuna siku utafanikiwa. Hii ni kwa sababu kama jambo uliloanzisha si hitajio la watu, maana yake hutapata wateja wa kununua bidhaa zako. Badala yake watafuata bidhaa ambazo ni hitaji lao. Kupitia njia ya kuchunguza itakuwezesha kufahamu wateja wako watakuwa kina nani. Usianzishe biashara kwa kutegemea yeyote atakayepita atanunua. Ndiyo yeyote atakayepita anaweza kununua lakini wale wateja wako uliowakusudia waendelee kuwapo.

Jambo la pili, epuka sana kuanzisha biashara inayofanywa na wengi katika eneo hilo. Unaweza kuwa unaishi mahala fulani, jirani yako anauza vitumbua na wewe ni mmoja wa wateja wake. Lakini kila siku unaona wateja ni wengi sana, wazo linalokuja kichwani mwako ni kwamba na mimi nikianzisha hapa, nitawapata kama yeye. Kitakachotokea kama utaanzisha maana yake mtagawana wateja, ikiwa alikuwa anapata Sh. 10,000 kwa siku mtagawana na mwisho wa siku wote mtashindwa kuendelea na biashara.

Jambo la tatu, usianzishe biashara ambayo hujawahi kuifanya kwa pesa za mkopo. Siku hizi umekuja mtindo wa vikoba, kupeana pesa kila baada ya muda fulani au unaamua kwenda benki kukopa fedha kwa ajili ya biashara ambayo ni ngeni kwako, hakika utajuta hapo baadaye usifanye hivyo.

Prof. Rostow aliyafananisha maendeleo kama ambavyo ndege inaanza kupaa, kwamba kabla ya kupaa na kupotelea mawinguni inaanza kidogo kidogo (Wajita tunaita Okusesela) kisha ndiyo inapaa au wengine wameyafananisha maendeleo kama ambavyo mtoto anakua, kwamba anatambaa, anasimama kwa kushikilia vitu na baadaye anaweza kusimama peke yake.

Biashara nayo inatakiwa kufuata sheria hiyo. Anza na mtaji mdogo ulio nao. Kwanza utaanza kujifunza namna unavyopata faida hata kama ni kidogo, lakini ukiweza kutunza hiyo faida ndogo na ukaweza kuikuza, basi katika biashara kubwa pia utafanya hivyo. Lakini zaidi unapoanzisha biashara usiyo na uzoefu nayo, wakati huku kwenye kikundi au benki wanasubiri marejesho, kuna hatari ya kushindwa biashara hiyo na kuna wakati unaweza kugombana na wateja, ukidhani tatizo ni wao. Hatukatai kukopa ni jambo jema, lakini kopa wakati biashara tayari unaifahamu, unajua faida yake na wateja wako.

Jambo la nne, ni juu ya eneo unaloanzisha biashara yako. Je, ni eneo rafiki kwa wateja wako kufika? Ndiyo maana utaona fremu nyingi ambazo ziko maeneo ya barabarani wamiliki wanatoza kodi kubwa kwa sababu wanaamini fremu ikikaa katika eneo la barabarani ni rahisi kuwapata wateja wale wa kudumu lakini pia wapita njia. Tano, utamaduni na hali ya eneo. Bidhaa utakazouza lazima uzingatie utamaduni na hali ya eneo husika. Usifungue biashara tu kwa sababu unataka kuonekana kwamba na wewe ni mchakarikaji na kwamba wenzako wakienda kazini na wewe unakwenda kwenye biashara, hivyo unaona aibu kubaki nyumbani kwa maana hiyo, bora ukae kwenye duka hata kama hakuna wateja.

Huwezi kufanya biashara ya nguruwe maeneo ambayo yametawaliwa na jamii ya Waislam au ukafanya biashara ya kanzu maeneo ambayo yametawaliwa zaidi na Wakristo.

Jambo la sita ni kuhusu uhakika wa bidhaa zenyewe. Kwanza, uhakika katika ubora, pili uhakika wa namna rahisi ya kuzipata kwa mwendelezo. Kwenye ubora wa bidhaa utakufanya uwe na wateja wa kudumu, wakishakuwa ni wa kudumu, maana yake hizo bidhaa zinatakiwa pia ziwe zinapatikana wakati wote. Hakuna jambo baya kwa mteja kumwambia bidhaa zimeisha njoo siku fulani. Ujue kuwa ueshamkosa huyo.

Jambo la saba kabla ya kuanzisha biashara uwe na uhakika wa lugha utakayokuwa unaitumia kwa wateja wako, bila kujali kwamba ni wachache au watakuwa wengi kiasi gani. Watanzania wengi tulivyo, huwa biashara ikiwa mpya na tupo katika harakati za kutafuta wateja huwa tuna tumia lugha nzuri sana, lakini tukishaona wateja wamezidi tunaanza lugha za dharau.

Chunguza tu migahawa mingi ikiwa mipya, hoteli na kadhalika baada ya muda tukishaona tumepata kafaida kidogo, mabega yote juu utaniambia nini! Tunaanza kupoteza mteja mmoja mmoja tena unamwambia “Kwani wewe usiponunua unafikiri sitauza”? Ebo! Hujui kwamba huyo atamwambia huyu na yule? Baadaye biashara zikiyumba tunaanza kiguu na njia kwa waganga wa jadi, unaanza kuona majirani zako ni wachawi kumbe wewe ndiyo mchawi wa biashara yako.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# ‘Dear X’ anavyonangwa na wasanii na kuonewa huruma na wanamuziki



Na Adam Fungamwango

KUACHANA kati ya mume na mke, au mtu na mpenzi wake hakukuanza leo, kupo tangu enzi na enzi.

Lakini huko nyuma hatukuona visa vingi watu wanaoachana kama hivi leo. Binadamu wanaachana na sababu tofauti ambazo zinawafanya wasiishi tena pamoja au kuwa wapenzi. Hili ni jambo la kawaida sana, lakini kwa miaka ya karibuni, yaani kizazi cha sasa unaweza ukadhani kuwa siku hizi ndiyo watu wanaoachana lakini zamani hawaachani.

Huko nyuma watu walikuwa wanakubali matokeo. Wanaachana kwa usalama. Na hata wakikutana watasalimiana na kuongea, lakini kwa wakati huo kila mtu tayari ana mtu wake. Lakini kwa sababu walishawahi kuishi pamoja na ni sababu tu za kimazingira au zozote zile zilizowafanya watengane, hazizuii wao kuwa kama watu wanaofahamiana.

Ndiyo maana ukifuatilia sana, utakuta huko nyuma waliotengana wengi walirudiana. Walirudiana kwa sababu wakati wanatengena hawakutukanana, kukashifiana, kutoleana siri na kudhalilishana. Kila mmoja alishindwa kuishi na mwenzake kwa sababu ambao waliziona kwa wakati huo, lakini kwa sababu wanaendelea kuwasiliana na kuulizana habari za kimaisha, baadaye huwa wanarudiana.

Wengine wanakuwa wameshazaa, kwa hiyo huwa wanakutana kwa ajili ya watoto, hivyo baadaye kila mmoja akikutana na mwenzake kuna mvuto fulani unatokea na kila mtu anaona huko alikokwenda hajapata furaha ile aliyokuwa akiipata kwa mwenzake.

Hakuna anayeweza kurudiana na mpenzi ambaye amekudhalilisha mbele za watu. Hakuna yoyote anayeweza kurudiana na ‘dear X’ wake ambaye alitoka nje na kusimama mlangoni akibwata majirani wasikie.

Siku hizi watu wakigombana na wapenzi wao kutokana na maendeleo ya teknolojia wanafuta hata namba za simu, kuondoka au kuwaondoa kwenye magrupu ya mitandao ya kijamii, wakifuta pia majina yao. Wako wanaochapisha kwenye mitandao ya kijamii mabaya yote ya mume, mke au mpenzi wake.

Siku hizi watu wameendelea zaidi wapo wanaotishia hata kuitisha mkutano wa waandishi wa habari kwa ajili ya kueleza eti kile kilichosababisha waachane.

Ikishafikia huku ni mbaya sana kwa sababu inatengeneza chuki. Zamani watu wakiachana kila mtu anabaki na lake kifuani. Hata kama kuna baadhi watakuwa wanajua au kudhani lakini wenyewe wapenzi au wanandoa wasiwe wathibitishaji. Iwe tumeachana tu. Hii ni kinga kubwa huko mbele ya safari kwa sababu maisha ni mzunguko.

Ukitaka kuona kuwa wapenzi wa zamani na sasa ni tofauti linalipokuja suala la kuachana sikiliza hata wanamuziki wa sasa wa miaka ya nyuma.

Mwanamuziki au msanii siku zote ni kama kioo, anaakisi kile ambacho kipo kwenye jamii kwa wakati huo.

Nyimbo za wasanii hawa wa kisasa, mawazo yao yanawakilisha kile ambacho kimo kwenye jamii ya sasa. Wakiimba tofauti hata watu watawashangaa.

Kuna ngoma moja ya msanii Mario inaitwa ‘Dear X.’ Yeye kwenye ngoma hii anasema kumrudia X wake, yaani mpenzi wake wa zamani ni bora ya kufa.

“Si ulinidharau, unakiona wa nini mama, na ukasahau kuwa vizuri vipo vingi, ukirudi umelewa, pole dear X mwenzako nipo salama, mambo stress nishasahau hizo zama, lako penzi feki kwangu nimechina, kwangu sizeeki, nadekezwa kama mwana.”

Huyo ni D Voice ngoma yake ‘X Wangu.’ Smile The Genius naye na ngoma kama hiyo ambayo ina mashairi haya hapa.

“Najua dua unazoniombea ni njema, najua unavyoumia, nishajisahaulia, huna faida, nanawiri, huyu niliyenaye ndiyo anayesababisha.”

Hiki ndiyo kizazi cha sasa. Kwao kuachana ni nongwa. Wanakuwa maadui kabisa. Wasanii hawa wanaleta kile ambacho kimo kwenye jamii kwa sasa. Ndiyo maana kuachana sasa imekuwa kama kitu cha ajabu kiasi kwamba watu wanawekeana visasi na hata kufikia kutoana roho.

Turudi kwa wanamuziki wa zamani nao walikuwa na kizazi chao cha wanaoachana. Wao walikuwa wanafanyaje? Wimbo wa ‘Pole Mkuu Mwenzangu’ wa DDC Mlimani Park unawakilisha hapa.

“Sitochoka kukwambia, hata kama tumeachana, wafitini hawachoki kuwakosanisha wapendanao. Mengi walikueleza na wewe hukuyachunguza, walisema eti mume gani anayekuweka kama pazia. Kuolewa ni utumwa natena ni kunyiwa starehe, hebu angalia sisi wenzako tunavyoyaponda maisha. Ulivyokwisha-shawishika, ukaanza dai talaka, nami nikakuruhusu, wende zako ukaishi salama.

Ilikubidi ufikiri ndipo uamue, bora kazia kuliko bendera kufuata upepo. Ninapopata habari zako nakusikitia, kutwa uko kwenye mabaa na kurandaranda na njia. Sasa tazama umecheza pata potea, pole mkuu mwenzangu kwa yote yanayokukuta.”

Huyu anamkumbusha ‘dear X’ wake sababu zilizosababisha wakaachana. Lakini pia anamuasa kuwa anachokifanya sasa kutwa kwenye mabaa si tabia nzuri, pia anampa pole kwa maswahibu yote yanayomkuta. Kwa maneno hata hawa wakienda sawa wanaweza hata kurudiana. Kwa sababu mwanaume anaonekana kumhurumia mkuu mwenzake na siyo yule anayesema “nimekutana na X wangu kakonda mbwa yule.”

Pia kuna wimbo wa Joyce uliopigwa na bendi ya Atomic Jazz.

“Ondoa mawazo yako, nimekwishakusamehe, mimi nakukuwa Joyce, usirudie tena, uliyoyafanya zamani ni mabaya sana, sasa yamewisha Joyce usirudie tena. Nakukanya mama ooo, usirudie tena, siku zote Joy, sasa rudi nyumbani ooo, usiteseke mama, yamekwisha Joy ooo, tutakuwa pamoja.”

Hawa ni Ma X ambao walikuwa wameshaachana, lakini hawakutengena kwa matusi na kudhalilishana, yamepitika maridhiano na tayari mwanaume anamsamehe na kumwambia arudi nyumbani ili asiendelee kuteseka na kuzurura mitaani. Hawa ndiyo wapenzi wa zamani, na wanamuziki wa zamani.


**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaji, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele. Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

# Harusi imevunjika - 14

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)




MAKUBWA we shoga yangu acha tu. Kwanza tayari nimeshakumaliza, angalia ulivyopendeza na hizo nywele zako."

Nasma akaangua kicheko cha kimbea. Akachukua kioo na kujitazama. Akaridhika na jinsi alivyojiona. Akatabasamu.

"James leo akiniona, hawezi kuniruhusu kuzurura hapa kijijini."

"Na alivyokuwa na wivu shemeji yangu yule loh!"

"Enhee tuendeleee na mastori yetu."

"Basi dada, mwanaume alikuwa tayari keshakolea, na kaniambia ataniona.

Tukawa tunabishana, atapelekaje tena barua wakati kuna barua ilishajibiwa na harusi ikataka kufanyika, nikamwambia muolewaji ni mimi na bado ndoa ilikuwa haijapita kwa hiyo, nikamshusha presha kaka wa watu kuwa barua yake itapokelewa tu na hata isipopokelewa upande wa baba, ipelekwe hata upande wa mama kwa wajomba zangu, wanaweza kusimamia tu mchakato nikaolewa, basi tukakubaliana na Jaziru wangu.

Sasa shoga kilichotokea. Ndiyo hicho ambacho kimenifanya leo unione nimekuja tena kuishi huku. Ingekuja labda kutembea tu, lakini siyo kurudi moja kwa moja."

"Hepo ndiyo nilikuwa napataka mimi."

"Mmmh! Mwangalie kwanza, yaani mpaka unakaa vizuri, maana unaona kama utakuwa husikii, naa wewe kwa umbea, ile ole wako nisikie hizi habari zimevuja hapa kijijini."

"Wala shoga yangu, mimi na wewe..."

"Hee, naogopa, habari hii ikijulikana sijui nitaweka wapi uso wangu. Sijui hata kama hapa tena ninaweza kuishi." Akasema Vayajo na kuendelea.

"Mama wee, tumeendelea na maisha. Maisha mazuri Naa. Maisha ya kifahari shoga yangu. Si unaona nilipokuja hapa siku za mwanzo nilivyonawiri?"

"Ni kweli shoga yangu, ndiyo maana mimi nikajua kabisa kuwa ulikotoka huko kumelipa. Ila nashangaa tu mpaka leo bado uko huku kijijini."

"Naa, siku isiyo na jina mwaya, saa nane na usiku tunasikia geti linagongwa. Mfanyakazi wetu kaenda kufungua wakaingia maaskari, wakasema wanamtaka mwenye nyumba.

Kutoka mama wakamuweka chini ya ulinzi. Mimi kilio shuu. 'Jamani mume wangu kafanya nini?' Wakaniambia mumeo anatuhumiwa kwa wizi, na kutakatisha pesa. Likanishuka. Wakaniambia yeye na wenzake wawili wanatuhumiwa kuiba kwenye kampuni wanayofanyia kazi zaidi ya shilingi milioni mia tatu, na pesa nyingi ambazo hawafahamu hata kiasi chake zimatakatishwa kwa hiyo wanamshikilia kwa uchunguzi."

> **"Sasa je. Walipoondoka, mimi hata sikulala, nilisubiri kuche tu niondoke maana nikajua huu sasa mkosi isije na mimi nikafuatwa asubuhi, maana mimi walinihesabu pale kama ni mkewe, naweza kuitwa kwa ajili ya hata mahojiano."**

Nasma alionekana kushtushwa na habari ile. "Kumbe mwaya. He pole sana shoga yangu kwa yaliyokukuta, hii ndiyo sababu iliyokufanya urudi kijijini?"

"Sasa je. Walipoondoka, mimi hata sikulala, nilisubiri kuche tu niondoke maana nikajua huu sasa mkosi isije na mimi nikafuatwa asubuhi, maana mimi walinihesabu pale kama ni mkewe, naweza kuitwa kwa ajili ya hata mahojiano."

"Ukaogopa kwenda kuisaidia polisi."

"Ya nini mie niingie kwenye msala usionihusu. Wizi kafanya yeye, mimi nilikuwa natumbua naye tu, niingizwe kwenye mkumbo wakati wale siyo mke au mchumba. Alfajiri jogoo hajawika mimi nikakusanya kilicho changu pale, uuuuuuuu, ndiyo hapa hadi leo hii inaniona hapa Msangani nimerudi."

"Mmmh, shoga yangu pole, sasa inakuje, maana hakuna pesa, hakuna uchumba, hakuna ndoa na huku ndiyo umeshaharibu."

"Yaani Naa kama mkosi. Maana Jaziru alivyoniita na nilipofika kule, nilijua kabisa nimeshawini, nimeshatoka kimaisha, wala haikuwa stori tena, baba alikuwa na pesa yule. Lakini kweli yule atakuwa mwizi maana mwanzoni nilivyomfahamu hakuwa vile, amezipata ghafla tu, alikuwa kapuku hadi nikamkataa nikamkubali Jerry.

"Kwani huyo baba na Jerry wewe uliyekuwa unampenda zaidi ni nani?"

"Bwana ee, kweli nimekimbia harusi yangu mwenyewe, lakini mimi nilifuata pesa na maisha mazuri kwa Jaziru, ila Jerry ndiyo yupo moyoni mwangu."

"Eeeeh dada we, uliyemkimbia siku ya harusi kabla ya ndoa haijapita..." Akaongea Nasma kama kwa kejeli hivi.

"Maisha ndugu yangu. Si nimekwambia ile kukimbia tu hapa ilikuwa ameshaniingizia shilingi milioni saba, na Zulfa alivyolazwa nilipopata taarifa nikamdanganya kuwa mama yangu amelazwa nataka nitume nyumbani akanipa shilingi milioni tatu.

Hata hapa nilipo kakamatwa tu lakini tayari kwenye akaunti yangu kuna shilingi milioni 10. Biashara yoyote ile sasa hivi naweza nikaifanya, hivi sasa nimetuliza kichwa tu kwanza ili nijue nitafanya nini."

"Jerry umeshaonana naye?"

"Mwenzangu hilo ndilo linaloniumiza kichwa."

"Vayajo, na aibu ile uliyompa baba wa watu unadhani unaweza kweli?"


"Unajua shoga yangu, hakuna mkate mgumu mbele ya chai. Yule Jerry nikikaa naye naye, nikalia, nikambembeleza, nikamuomba radhi, tena nikimwambia nina shilingi milioni kumi benki tuanzishe biashara au mradi wowote, sijui kama atakataa."

"Mmmh, inawezekana mwaya."

"Ila dada we, kuna kitu kimeingia kati hapa, naona kama itakuwa kazi kubwa kushawishi mpaka kukubali. Isingekuwa hivyo kazi yangu ingekuwa rahisi tu."

"kitu gani hicho?"

ITAENDELEA JUMAPILI



# LADY JAY DEE, RAMA DEE KUANDAA SHOO KIFALME

WANAMUZIKI wakongwe Lady Jay Dee na Rama Dee wanatarajia kufanya shoo ya kipekee itakayonguruma kwa jina la 'Love Sentense' katika ukumbi wa Milimani City Dar Es Salaam.

Shoo hiyo ambayo imetajwa kuwa na hadhi ya juu, itakuwa na viingilio vya watu maalumu pekee.

Kwa mujubu wa Lady Jay Dee, burudani hiyo ambayo itakuwa maalumu ya kufungua mwaka, itafanyika mwishoni mwa mwezi huu.

Wasanii hao wanafanya vyema na kibao chao 'Matozo' moja kati ya kazi ambayo itakuwa katika albamu ya pamoja.

# Baba Levo akoleza utambi

SAKATA la wasanii wa muziki wa kizazi kipya Diamond na Marioo, linazidi kuibua sura mpya baada ya mchekeshaji na mwanamuziki, Baba Levo kusema kolabo ya wawili hao sijui kama itatoka kutokana na hali kuwa mbaya.

Baba Levo amesema kitendo cha Marioo kueleza kuwa Diamond aliteleza kuongea hadharani, kimemkasirisha msanii huyo kwa kuonekana yeye ni muongo.

"Diamond amechukizwa na kauli ile ya Marioo na inaonyesha amemwambia muongo wakati ilikuwa kweli alichoongea sidhani kama kolabo ambayo tayari ilisharekodiwa itatoka," amesema Baba Levo.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NEVES ATAJWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inafikiria kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Ureno, Ruben Neves, 25, ambaye amebakiza miezi 18 kwenye mkataba wake wa sasa pale Wolves. ***(Mail)***

### POTTER IPO NA CHELSEA

CHELSEA inamuunga mkono kocha wake, Graham Potter na wanapanga kuwakata mishahara wachezaji wa timu hiyo kama matokeo wanayopata hayataimarika. ***(Telegraph)***

### MUDRYK KUTUA ARSENAL

ARSENAL inajiamini kukamilisha usajili wa pauni milioni 80 wa Mykhailo Mudryk, 22, kutoka Shakhtar Donetsk kwa wakati na kumfanya winga huyo wa Ukraine kuanza kuichezea dhidi ya Manchester United wiki ijayo. ***(Times)***

### THURAM KUSAJILIWA CHELSEA

CHELSEA inaweza kumsajili fowadi wa Ufaransa, Marcus Thuram, 25, kwa ada ya euro milioni 10 mwezi huu kutoka Borussia Monchengladbach, huku mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Caught offside)***

### AMRABAT AITAKA ATLETICO

LIVERPOOL imekutana na wawakilishi wa Sofyan Amrabat, 26, kujaribu kumshawishi kiungo huyo wa Fiorentina kuhamia Anfield, lakini mchezaji huyo raia wa Morocco anataka kwenda Atletico Madrid. ***(Mirror)***

### TROSSARD NJIA MOJA

CHELSEA na Tottenham Hotspur zinamfuatilia kwa karibu, Leandro Trossard, 28, baada ya wakala wa winga huyo wa Ubelgiji kutoa taarifa mchezaji huyo anataka kuondoka Brighton. ***(Football.London)***

### MATAJIRI WAIGOMBEA UTD

MANCHESTER United imepokea ofa ya kununuliwa kutoka Mashariki ya Kati, Asia na Marekani na inataka ofa rasmi mwezi ujao. Bilionea wa England, Sir Jim Ratcliffe pia anatarajia kutoa ofa ya kuinunua klabu hiyo. ***(Telegraph)***

### MADUEKE ANUKIA CHELSEA

CHELSEA ipo kwenye mazungumzo na PSV Eindhoven kuhusu uhamisho wa winga wa Timu ya Taifa ya England, Noni Madueke, 20. ***(Football.London)***

### YAMTAKA MONTEIRO

KLABU za Everton na Wolves zinamwania mlinzi wa Brazil, Felipe Monteiro, 33, ambaye amebakiza miezi sita kwenye mkataba wake na Atletico Madrid. ***(Mail)***

### GOMES SAFI WOLVES

KLABU ya Wolves imekubali dili la kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Brazil mwenye umri wa miaka 21, Joao Gomes kutoka Flamengo. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: ARSENAL INATAKIWA KUJIDHIBITI IKIWAVAA SPURS

**LONDON,** England

**Kocha huyo afunguka mechi ya leo ni mtihani mwingine kwa kikosi chake...**

KOCHA Mikel Arteta amekiri Arsenal inahitaji kudhibiti hisia zao zaidi baada ya kukabiliwa na mashtaka mfululizo kutoka katika Chama cha Soka cha England (FA).

**Washikabunduki hao walitozwa faini ya pauni 40,000 hapo juzi kwa kushindwa kuwadhibiti wachezaji wao katika suluhu dhidi ya Newcastle United, baada ya kudai kunyimwa penalti ya dakika za mwisho kwenye Uwanja wa Emirates.**

Shtaka lingine likaja kwa upande wa Arteta kwa kukata rufani katika ushindi wa raundi ya tatu ya Kombe la FA dhidi ya Oxford United, huku tabia ya Arsenal katika mechi zote mbili ikionyesha ya uvotu wa nidhamu.

Mchezo wa leo 'dabi' ya London Kaskazini dhidi ya Tottenham Hotspur utatoa mtihani mwingine wa uwezo wa Arsenal kudhibiti hasira zao, huku wakitafuta kudumisha nafasi yao kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England.

Arteta alikabiliwa na maswali kuhusu mashtaka katika mkutano wake na waandishi wa habari, ingawa alikiri timu inahitaji kufanya vyema katika kipengele hicho, anahisi hawezi kudhibiti hisia zake mwenyewe.

"Ninajali sana heshima ya klabu yangu, siwezi kuidhibiti," alisema.

"Ninajaribu kufanya niwezavyo kuwatetea wachezaji, kutetea klabu na hiyo inakuja kwa watu fulani ambao hawataipenda. Kwa hakika, ikiwa kila mtu angependa, haitakuwa nzuri sana.

"Sio sijali ila najali sana hasa ninapofanya kazi zangu, nikiwa nimekaa nyumbani huwa namjali mke wangu anawaza nini na watu wanawaza nini lakini wewe hujui.

"Lakini ninapokuwa hadharani, ninajali sana kuhusu nini tunaweza kufanya vyema kwa klabu na bora zaidi kuwatetea wachezaji. Na hili ni jukumu langu pia.

"Ninakubali tunapaswa kudhibiti kile tunachoweza kudhibiti na kuna mambo fulani ambayo tunaweza kufanya vizuri zaidi.

"Hivyo ndivyo timu kubwa hufanya na inayofuata imekwisha na unaweza kutoka sare au kupoteza na inaweza kumaanisha hali tofauti sana."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
REAL MADRID
VERSUS
BARCELONA
1 | 2.65
X | 3.45
2 | 2.47

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# EVRA ATAKA MCCARTHY APEWE SIFA ANAZOSTAHILI



**MANCHESTER,** England

MLINZI wa kushoto wa zamani wa Manchester United, Patrice Evra, ametaka kocha wa washambuliaji wa timu hiyo, Benni McCarthy kupewa sifa zake anazostahili.

Evra anaamini kazi kubwa ya kuwabadilisha washambuliaji ndani ya United anaifanya kocha huyo.

McCarthy amekua kocha wa washambuliaji wa United tangu mwazoni mwa msimu huu akitokea Amazulu ya Afrika ya Kusini.

Kuna mabadiliko makubwa kwa washambuliaji wa United ambao wamekua wakifunga kwa ustadi mkubwa katika michezo tofauti msimu huu.

Lakini sifa bado haziendi kwa McCarthy kitu ambacho Evra anaona sio sahihi.

Marcus Rashford ni miongoni mwa washambuliaji waliokua na mabadiliko makubwa msimu huu tofauti na msimu uliopita.

Msimu huu Rashford amefunga mabao kwa ustadi na hiyo inaonekana ni matokeo ya Mccarthy.

Kwani tangu kuja kwa kocha huyo ndani ya klabu hiyo mwanzoni mwa msimu yameweza kumbadilisha kwa kiwango kikubwa mshambuliaji huyo ambaye amehusika kwenye mabao 21 hadi sasa.



## *Hatimaye Mendy hana hatia*

**MANCHESTER,** England

MCHEZAJI wa Manchester City, Benjamin Mendy, hajapatikana na hatia ya makosa sita ya ubakaji na moja la unyanyasaji wa kingono yaliyokuwa yakimkabili.

Majaji hawakupata ushahidi wa kufikia uamuzi kuhusu shtaka moja la ubakaji na lile la kujaribu kubaka, baada ya kesi iliyodumu kwa miezi sita katika Mahakama ya Chester Crown.

Hata hivyo, upande wa mashtaka ulitaka kusikilizwa upya kwa makosa hayo.

Louis Saha Matturie, mwenye umri wa miaka 41 pia hakupatikana na hatia ya makosa matatu ya ubakaji.

Majaji walishindwa kutoa uamuzi kwa makosa matatu ya ubakaji na makosa matatu ya unyanyasaji wa kingono dhidi yake.

Mendy na rafiki yake Matturie walikuwa wameshtakiwa kwa ubakaji na wanawake katika nyumba ya mchezaji huyo huko Prestbury, Cheshire, Manchester.

Y | CHEZA USHINDE KASINO

# YACOUBA AWAAGA YANGA, MUSONDA AKITAMBULISHWA

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI Yacouba Songne, ambaye ni raia wa Burkina Faso jana amewaaga rasmi wanachama na mashabiki wa Yanga baada ya klabu hiyo kumtambulisha straika mpya, Kennedy Musonda (pichani) aliyetokea, Power Dynamos ya Zambia.

**Kupitia mtandao wake wa kijamii ya Instagram, Yacouba ambaye kwa msimu mzima alikaa nje kutokana na kuwa majeruhi, aliandika waraka wa kuwashukuru na kuwaaga mashabiki wa Yanga kwa wema wote waliomtendea tangu alipofika.**

"Ulikuwa wakati mzuri tangu tulipokuwa pamoja mpaka sasa, asanteni kwa upendo wenu kwangu na ushirikiano kuanzia kwa wachezaji hadi uongozi wote wa Yanga, daima nitawakumbuka hadi wakati mwingine, wananchi asante sana na kwaherini nawapenda," aliandika mchezaji huyo anayemudu kuchezea nafasi ya mshambuliaji na winga.

Yanga ilimsajili mchezaji hiyo Agosti, mwaka 2020 akitokea Asante Kotoko ya Ghana, hata hivyo alitumia kipindi kirefu kuwa majeruhi kuliko uwanjani, baada ya kuumia Novemba 2, 2021, katika mechi dhidi ya Ruvu Shooting iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Aliumia dakika ya 31 na nafasi yake kuchukuliwa na Saido Ntibazonkiza ambaye kwa sasa yupo na kikosi cha Simba, Yanga ikiondoka na ushindi wa mabao 3-1. Madaktari walibainisha mchezaji huyo aliumia goti na kulazimika kupelekwa Tunisia kwa matibabu, ambapo klabu yake ililazimika kuendelea kumhudumia licha ya msimu huu hayupo kwenye orodha ya wachezaji 12 wa kigeni.

Kabla ya kuaga, tayari Yanga ilikuwa imemtambulisha Musonda ambaye alikuwa nchini kwa muda sasa, huku taarifa zikizihusisha kutua kwa watani wao wa jadi, Simba.

Straika huyo ametambulishwa kwenye mitandao mbalimbali rasmi ya klabu hiyo, akitajwa ndiye msaidizi wa Fiston Mayele kwenye safu ya ushambuliaji ya kikosi hicho ambacho kinajipanga kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na kufanya vizuri kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hadi anaondoka kwenye Ligi Kuu Zambia, alikuwa amepachika mabao 11 katika mechi 17 alizocheza.




## Beki kukamilisha hesabu

INATOKA UK. 24

alisema Hersi.

Naye Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema wanaendelea vyema na maandalizi kuelekea michezo iliyoko mbele yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kaze alisema kikosi cha timu hiyo kinajiimarisha kwa sababu kinafahamu michezo yote inayowakabili ni migumu lakini kwa sasa wanaiangalia zaidi Ihefu na wamejipanga kulipiza kisasi kwa kupata matokeo mazuri.

"Jumatatu tuna kazi kubwa ya kutafuta matokeo mazuri katika mchezo wetu dhidi ya Ihefu, wako vizuri walitufunga mechi ya mzunguko wa kwanza, tunahitaji kuwa makini katika maandalizi yetu, mabeki na washambuliaji wanatakiwa kucheza kwa tahadhari, wako nafasi za chini katika msimamo lakini hatuwezi kuwadharau," alisema Kaze.

Aliongeza wameona timu zote zimeboresha vikosi vyao kwa kusajili wachezaji wapya ikiwamo Ihefu, hivyo mechi za hatua ya lala salama zitakuwa na ushindani zaidi.

Kitendawili cha nani atacheza wapi katika mzunguko wa mwisho kitateguliwa leo saa 5:59 usiku wakati dirisha dogo la usajili litakapofungwa rasmi.

Musonda ametua Yanga akitokea nchini kwao Zambia katika klabu ya Power Dynamos na ataungana na Fiston Mayele katika safu ya ushambuliaji.

## *Mashabiki jiandaeni*

INATOKA UK. 24

rika, kwa hiyo kuna kazi ya kufanya kukiandaa kikosi, uzuri wachezaji wanashika mafunzo haraka," alisema Robertinho.

Simba leo itaweka rekodi yake nyingine kwa kucheza dhidi ya timu hiyo ya barani Ulaya, mechi itakayoanza saa 10:00 jioni kwa saa za Tanzania.

CSKA Moscow nayo ipo, Abu Dhabi Falme za Kiarabu kwa kambi ya muda mfupi kama ilivyo Simba ambayo iliyotolewa mapema kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi.

Mei 27, 2019, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Simba ilicheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Sevilla kutoka Hispania na kumalizika kwa kipigo cha mabao 5-4.

Baada ya mechi hiyo itaanza safari ya kurejea jijini Dar es Salaam kwa ajili ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na itaanza kwa kukutana na Mbeya City, Januari 18, mwaka huu.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAPILI - 15/01/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4363 | Umraniyespor vs Istanbulspor | 1.96 | 3.59 | 3.49 |
| 13:30 | 4569 | Tuzlaspor vs Adanaspor | 2.18 | 3.30 | 2.96 |
| 14:00 | 5263 | CD Feirense vs Viseu | 2.38 | 3.11 | 2.91 |
| 14:15 | 1011 | Vitesse Arnhem vs NEC Nijmegen | 2.12 | 3.37 | 3.22 |
| 14:30 | 4979 | Sassuolo vs Lazio | 3.13 | 3.43 | 2.13 |
| 15:00 | 1060 | Lille vs Troyes | 1.39 | 4.78 | 6.77 |
| 15:30 | 2021 | Brugge vs Anderlecht | 1.96 | 3.57 | 3.52 |
| 16:00 | 3001 | Eibar vs Malaga | 1.62 | 3.46 | 5.74 |
| 16:00 | 5422 | Getafe vs Espanyol | 2.49 | 2.94 | 3.04 |
| 16:00 | 5561 | Yeni Malatyaspor vs Bodrumspor | 3.55 | 3.26 | 1.96 |
| 16:30 | 1794 | Fortuna Sittard vs PSV Eindhoven | 7.75 | 5.16 | 1.32 |
| 16:30 | 3685 | GO Ahead Eagles vs Utrecht | 2.77 | 3.36 | 2.37 |
| 16:30 | 5104 | Moroka Swallows FC vs TS Galaxy FC | 2.75 | 2.80 | 2.90 |
| 17:00 | 1156 | Udinese vs Bologna | 1.92 | 3.37 | 3.81 |
| 17:00 | 1419 | AEK Athens vs Panetolikos | 1.14 | 7.18 | 17.94 |
| 17:00 | 1994 | Torino vs Spezia | 1.62 | 3.72 | 5.16 |
| 17:00 | 2343 | Angers vs Clermont Foot | 2.35 | 3.35 | 2.85 |
| 17:00 | 2411 | Newcastle vs Fulham | 1.49 | 4.27 | 5.75 |
| 17:00 | 2840 | Nacional Madeira vs CF Estrela | 2.61 | 3.30 | 2.51 |
| 17:00 | 3004 | Toulouse vs Brest | 1.96 | 3.54 | 3.54 |
| 17:00 | 4245 | Chelsea vs Crystal Palace | 1.66 | 3.66 | 4.85 |
| 17:00 | 5169 | Montpellier vs Nantes | 2.48 | 3.34 | 2.69 |
| 17:00 | 5970 | Reims vs Nice | 2.42 | 3.18 | 2.88 |
| 18:00 | 1609 | AEK Larnaca vs Aris Limassol | 2.25 | 3.24 | 3.14 |
| 18:00 | 1983 | KAA Gent vs Kortrijk | 1.35 | 4.98 | 7.37 |
| 18:00 | 2819 | Rangers vs Aberdeen | 1.52 | 4.29 | 4.78 |
| 18:15 | 1710 | Almeria vs Atletico Madrid | 4.61 | 3.71 | 1.71 |
| 18:15 | 3011 | Mirandes vs Lugo | 1.96 | 3.08 | 4.07 |
| 18:15 | 4256 | Ternana vs Ascoli | 2.18 | 3.22 | 3.22 |
| 18:30 | 4168 | GD Chaves vs FC Arouca | 2.15 | 3.23 | 3.33 |
| 18:30 | 4646 | Maritzburg Utd vs Bloemfontein Celtic | 2.60 | 3.00 | 2.85 |
| 18:45 | 2338 | Groningen vs Feyenoord | 6.13 | 4.45 | 1.44 |
| 18:45 | 5117 | Emmen vs Cambuur | 2.11 | 3.33 | 3.28 |
| 19:00 | 4219 | Morocco vs Sudan | 1.70 | 3.45 | 5.20 |
| 19:00 | 4624 | Gaziantep BB vs Fenerbahce | 4.78 | 3.88 | 1.64 |
| 19:05 | 5453 | Monaco vs AC Ajaccio | 1.39 | 4.58 | 7.17 |
| 19:30 | 4532 | Tottenham vs Arsenal | 3.03 | 3.32 | 2.23 |
| 20:00 | 1515 | Apollon Limassol vs Anorthosis Famagusta | 1.94 | 3.31 | 3.96 |
| 20:00 | 4563 | Atalanta vs Salernitana | 1.36 | 4.95 | 7.13 |
| 20:30 | 2872 | Olympiakos vs Aris Salonica | 1.37 | 4.27 | 8.94 |
| 21:00 | 1703 | Benfica vs Sporting Lisbon | 1.75 | 3.78 | 4.18 |
| 21:00 | 3074 | Oliveirense vs Belenenses | 2.22 | 3.31 | 3.01 |
| 21:15 | 1668 | Maccabi Haifa vs Hapoel Katamon | 1.26 | 5.06 | 8.95 |
| 21:30 | 4020 | PAS Giannina vs Panathinaikos | 7.17 | 3.43 | 1.55 |
| 22:00 | 5023 | Real Madrid vs Barcelona | 2.65 | 3.45 | 2.47 |
| 22:00 | 5617 | Botafogo RJ vs Audax Rio EC RJ | 1.53 | 3.80 | 5.46 |
| 22:00 | 5689 | Madagascar vs Ghana | 4.31 | 3.16 | 1.92 |
| 22:45 | 2580 | Roma vs Fiorentina | 1.95 | 3.36 | 3.71 |
| 22:45 | 4300 | Rennes vs Paris St Germain | 4.90 | 4.15 | 1.59 |
| 23:30 | 4090 | Porto vs Famalicao | 1.17 | 6.57 | 13.94 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Januari 15, 2023

Nipashe



**Hatimaye Mendy hana hatia** UKURASA 22



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimkabidhi kombe la ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi, nahodha wa Mlandege FC, Abdulnasir Assaa 'Gamal' baada ya kutwaa ubingwa huo juzi usiku. Mlandege iliwafunga Singida Big Stars mabao 2-1. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Simba: Mashabiki jiandaeni kufurahi

**Na Adam Fungamwango**

●●● Ni kauli iliyotolewa na bosi wa klabu hiyo ambayo leo inaivaa CSKA Moscow...

WAKATI leo ikitarajia kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya CSKA Moscow ya Urusi, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again' amewataka mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kujiandaa kufurahi zaidi.

**Kauli hiyo ya Try Again imetolewa zikiwa zimesalia saa chache kabla ya kufungwa kwa dirisha dogo la usajili ifikapo leo saa 5:59 usiku.**

Hata hivyo pia bado kukiwa na sintofahamu ya hatima ya kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto' aliyevunja mkataba na Yanga lakini watani hao wakitangaza kumsajili mshambuliaji Mzambia, Kennedy Musonda, ambaye alikuwa anawindwa na Simba.

Yanga imemsajili Musonda kwa kumpa mkataba wa miaka miwili na hivyo kuchukua nafasi ya Yacouba Sogne ambaye naye jana aliwaaga rasmi mashabiki wa klabu hiyo inayoongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Bosi huyo wa Simba aliliambia gazeti hili klabu yake haiwezi kumkosa mchezaji iliyemdhamiria kwa sababu imejipanga kuboresha kikosi chake kwa lengo la kufanya vyema katika Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.

"Wa mwisho kufurahi, hufurahi zaidi. Mtafurahi kweli kweli," Try Again alisema kwa kifupi.

Naye Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' ameonyesha kufurahishwa na viwango vya wachezaji wa timu yake licha ya kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Al Dhafra ya Falme za Kiarabu katika mechi ya kirafiki iliyochezwa juzi mjini Abu Dhabi.

Robertinho alisema wachezaji wake walionyesha viwango vya hali ya juu katika mechi hiyo, huku akiwashuhudia kwa mara ya kwanza wachezaji tegemeo wa kikosi hicho ambao hawakucheza michezo ya Kombe la Mapinduzi iliyomalizika kwa wenyeji Mlandege kutwaa ubingwa hapo juzi usiku.

"Leo nimekijaribu kikosi changu, nimewaona kwa mara ya kwanza baadhi ya wachezaji tegemeo, nimefurahia sana viwango vyao. Wachezaji wangu katika mechi hii wamecheza vizuri sana, tumezuia vizuri, tumeshambulia muda mwingi mwa mchezo, tumeingia katika eneo la wapinzani mara nyingi, kufungwa ni matokeo ya mchezo. Lakini kwa ukweli tumecheza vizuri sana, huu kwangu ni mwanzo mzuri kuona vijana wamecheza kwa kiwango hiki kwa siku nne tu ambazo nimeanza kufundisha," alisema Robertinho.

Kocha huyo alisema anaamini muda unavyozidi kuendelea atakuwa na kikosi imara ingawa anajua ana straika mmoja ambaye ni majeruhi.

Kuhusu mechi ya leo, kocha huyo alisema bado ataitumia kuangalia wachezaji wake na kutengeneza mifumo anayoifundisha licha ya kuwa anakutana na timu kubwa na maarufu barani Ulaya.

"Hata timu tuliyocheza nayo Al Dhafra ni ngumu pia, kwa sasa tunatengeneza kikosi kwa ajili ya mechi za Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Af-

INAENDELEA UK. 23

## Beki kukamilisha hesabu za Yanga

**Na Saada Akida,** ZANZIBAR

BAADA ya kumtambulisha straika mpya Mzambia, Kennedy Musonda, uongozi wa Yanga umesema unajipanga kukamilisha mazungumzo ya kumsajili beki wa kati, Mamhadou Doumbia, kutoka nchini Mali, imeelezwa.

Musonda amesaini mkataba wa miaka miwili na vinara na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga.

Rais wa Yanga, Hersi Said, aliliambia gazeti hili klabu yao inafanya usajili kwa kufuata mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti ya benchi la ufundi linaloongozwa na Mtunisia, Nesreddine Nabi na si vinginevyo.

Hersi alisema wamefurahi kumpata Musonda lakini kabla ya dirisha la usajili halijafungwa, watatetemesha nchi kwa kukamilisha usajili wao wa beki wa kati mwenye ubora wa hali ya juu.

"Bado tunaendelea kuboresha kikosi chetu kulingana na mahitaji tuliyokuwa nayo, tumekamilisha usajili wa Musonda sasa mashabiki wanatakiwa kuendelea kufuatilia mitandao yetu, kuna kifaa kingine kitatua kuitumikia Yanga kabla ya dirisha la usajili halijafungwa,"

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >